# Nipashe

Jumanne Aprili 23, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579899

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## CAG Assad abaini kufichwa maslahi, mikopo ya vigogo

UKURASA 2




UKURASA 13

# Timu kuchunguza simu, 'unga' gerezani yaundwa

UKURASA 2



NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI, HAMAD MASAUNI

## 'Hekima ilikosekana shauri la CAG Assad'

UKURASA 4



## Chadema wataka haki uchaguzi serikali za mitaa

UKURASA 3

**MICHEZO** AUSSEMS AICHAMBUA ALLIANCE, AITAJA YANGA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# CAG Assad abaini kufichwa maslahi, mikopo ya vigogo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini baadhi ya halmashauri nchini kuficha taarifa zinazohusu maslahi na mikopo ya viongozi wake wa juu.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18, CAG Assad anasema amebaini changamoto hiyo katika halmashauri tano za Wilaya ya Arusha, Mji wa Ifakara, Wilaya ya Korogwe, Wilaya ya Malinyi na Wilaya ya Ulanga.

Prof. Assad anaeleza kuwa aya ya kwanza ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma Na. 20 inaelekeza taasisi inayoandaa taarifa za fedha kwa msingi wa miamala isiyohusisha fedha taslimu (Accrual Basis), inawajibika kuonyesha taarifa za miamala inayohusu viongozi wakuu wa taasisi husika.

"Katika ukaguzi wa mwaka huu, nilibaini halmashauri tano hazikuonesha taarifa za viongozi wa juu wa halmashauri kuhusiana na maslahi yao, mikopo na malipo mengine yanayofanana na hayo, hivyo watumiaji wa taarifa za fedha za halmashauri wanaweza wasipate taarifa muhimu zinazoweza kuwasaidia katika kufanya uamuzi," anabainisha.

"Ninapendekeza kwamba, halmashauri husika zionyeshe taarifa za viongozi wake kama inavyotakiwa na aya ya kwanza

INAENDELEA UK. 8




Muuza dagaa wa kukaanga akiwa na ndoo iliyosheheni bidhaa hiyo akitoka katika soko la samaki la Feri jijini Dar es Salaam jana. Biashara hiyo imeajiri wanawake wengi. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Timu ya kuchunguza matumizi simu, 'unga' gerezani yaundwa

**Na Romana Mallya**

BAADA ya kubaini uwapo wa changamoto ya baadhi ya wafungwa kutumia simu na dawa za kulevya wakiwa gerezani, serikali imeunda timu ya kuchunguza uingizwaji wa vitu hivyo gerezani.

Machi 22, mwaka huu, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, akiwa ziarani mkoani Mbeya, aliagiza kuundwe timu ya kuchunguza kadhia hiyo na maofisa wanne waliodaiwa kuhusika, wasimamishwe kazi.

Akizungumza na Nipashe jana, Masauni alisema tayari timu ya kuchunguza suala hilo katika Gereza la Ruanda mkoani Mbeya imeshaundwa na inaendelea na kazi.

Masauni alisema anaamini ripoti ya timu hiyo itatoa ufumbuzi wa kudumu wa changamoto hiyo.

"Tayari maagizo yangu niliyotoa siku ile yametekelezwa na mengine yanaendelea kutekelezwa, niliagiza baadhi ya maofisa waliohusika wasimamishwe kazi, utekelezaji wake umeshafanyika, wapo maofisa kadhaa wamesimamishwa kazi," Masauni alibainisha. Naibu waziri huyo aliongeza: "Niliagiza kuundwe tume ya uchunguzi, imeshaundwa na sasa inaendelea na utekelezaji, tume imechukua muda kwa sababu tunataka tupate ufumbuzi wa kudumu wa masuala ya uingizaji simu magerezani na matumizi ya dawa za kulevya ambayo ni kinyume cha sheria."

Alisema tayari maofisa kadhaa wa magereza wamesimamishwa kazi kutokana na matukio hayo, akibainisha kuwa simu tisa na dawa za kulevya aina ya bangi alizikamata siku ya ziara yake.

"Maagizo yangu yametekelezwa na wale nilioagiza wasimamishwe kazi siku ile wameshasimamishwa, kwa sasa tunasubiri mapendekezo ya tume," Masauni alisema. Siku ya ziara mkoani Mbeya, Masauni aliagiza Inspekta Longino Mwemezi, Ramadhan Mhagama, Alexander Mwinjano na Benjamini Malango ambao wote ni masajini taji wa magereza, wasimamishwe kazi kupisha uchunguzi.

Alisema alibaini wafungwa wanamiliki simu tisa na kuna uingizwaji wa dawa za kulevya aina ya bangi ndani ya gereza, akieleza kuwa uingizwaji wake unafanyika kwa ushirikiano kati ya askari wasiokuwa waaminifu na wafungwa.

Alisema vitendo vya aina hiyo vilishakemewa na Rais John Magufuli na aliagiza vidhibitiwe ndani ya magereza yote nchini ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

Alisisitiza kuwa vitendo hivyo ni hatari kwa usalama wa magereza endapo askari wataendelea kutokuwa waaminifu kwa kuruhusu viendelee kufanyika ndani ya magereza.

Naibu Waziri Masauni aliwataka wakuu wa magereza yote nchini kuwa makini kwa kuzuia vitendo hivyo vya ukiukwaji wa sheria na maadili ili kulinda usalama wa maeneo hayo ambayo ni hatarishi.

## Watano ajali ya Arusha hali mbaya

**Na Waandishi Wetu**

WATU wawili wamekufa papo hapo na wengine watano hali zao ni mbaya baada ya magari waliyokuwa wakisafiria kugongana eneo la Oldonyo Sambu mjini Arusha.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Jonathan Shana, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo juzi saa tisa alasiri na kueleza kuwa waliofariki mmoja ni raia ya Kenya na mwingine Tanzania.

Aliwataja waliofariki kuwa ni dereva Onesmo (20), raia wa Kenya ambaye alikuwa akiendesha gari lenye namba za usajili KCH 665G aina ya Mistubish Saloon ambaye alikuwa na abiria Peter Donald ambaye ni Mtanzania.

Kamanda Shana alitaja gari lingine ambalo liligongana na hilo kuwa ni T 612 ENE aina ya Toyota Saloon ambayo wakati huo madereva wote walikuwa wakielekea kwenye kikao chao cha mashindano ya magari na siyo kweli walikuwa katika mashindano.

Alisema katika ajali hiyo watu wengine watano walijeruhiwa na hali zao ni mbaya na wote wamepelekwa Hospitali ya Seliani kwa matibabu.

"Waliojeruhiwa ni Arnoldo's Twahili, Bosco Mshanga (29), Clara na Stella Musoni (21) ambaye ni raia wa Kenya," alisema.

Alisema ajali hiyo ilitokea wakati dereva wa Toyota Saloon alipokuwa akikata kulia kuelekea Ngarinanyuki, huku dereva wa Mistubish Saloon aliyekuwa nyuma ya gari hilo naye wakati huo huo akitaka kulipita ndipo alipokwenda kuligonga ubavuni.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kutembelea majeruhi, Kamanda Shana alirusha lawama kwa watumiaji wa mitandao ya kijamii ambao walipotosha ukweli kwa kudai waliofariki ni watu nane na walikuwa kwenye mashindano ya magari.

Kamanda Shana aliukumbusha umma kuwa waache tabia ya kutoa taarifa bila kuzithibitisha kwa mamlaka husika kwa sababu kwa kufanya hivyo ni kuzua taharuki kwa ndugu, jamaa na marafiki.

Pia Kamanda huyo alisisitiza kuwa kuanzia sasa watakuwa wakali zaidi ya pilipili au sumu kwa madereva ambao hawataki kufuata sheria za usalama barabarani.

"Katika tukio hili lililosababisha majeruhi watano na wawili wamefariki, majeruhi hali zao ni mbaya," alisema Kamanda Shana.

Pia alitoa wito kwa madereva wote wawe makini wanapoendesha vyombo vya moto na kuwaonya wanaotumia vileo.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alikanusha idadi iliyotajwa mtandaoni kuwa waliofariki ni raia nane kutoka Kenya na kueleza kuwa taarifa hiyo imeleta taharuki kwa ndugu.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya madaktari, majeruhi hao waliumia sehemu za kichwa na uti wa mgongo na mmoja wao amelaza katika chumba cha wagonjwa mahututi baada ya kupoteza fahamu.

Aidha, alisema majeruhi hao wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Seliani na hali zao zinaendelea vizuri, isipokuwa mmoja wao aliyelazwa chumba cha wagonjwa mahututi.

"Nawaomba Watanzania tatizo linapotokea msubiri kupokea taarifa kutoka katika mamlaka husika," alisema Muro.

**Imeandikwa na Romana Mallya (Dar) na Allan Isack (Arusha)**



Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyabaganga Taraba, akipanda mti katika ofisi ya Kata ya Shangihilu kwenye siku ya Tamasha la Kupinga Mila na Desturi Kandamizi ambazo zimekuwa zikisababisha kukithili kwa mimba na ndoa za utotoni, lililoandaliwa na Shirika la Save The Children, **PICHA: MARCO MADUHU**

# Marufuku kamata mifugo hifadhini bila mchungaji

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewaagiza maofisa wanyamapori wanapokamata mifugo itakayokutwa hifadhini wahakikishe pia wanawakamata wachungaji wa mifugo hiyo.

Agizo hilo limetolewa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akisema kuwa mifugo mingi inayokutwa hifadhini imekuwa ikikimatwa bila wachungaji wakidaiwa kukimbia.

Uamuzi huo umetokana na tuhuma za rushwa zinazowakabili baadhi ya maofisa wanyamapori kuwa baada ya kuikamata mifugo hiyo ikiwa hifadhini huwaruhusu wachungaji wakatafute pesa za kuwahonga ili waiachie mifugo hiyo na wanaposhindwa kuzipata pesa walizokubaliana hushindwa kuirudia mifugo yao kwa hofu ya kukamatwa.

"Wekeni kambi hapo hapo mahali mtakapoikuta mifugo hadi pale mmiliki wa mifugo au mchungaji atakapojisalimisha, awe amejificha na kama amepanda juu ya mti mfuateni, ninyi ni askari tuliowaamini," alisema Kanyasu.

Ametoa agizo hilo alipokuwa akizungumza na mameneja na watumishi wa mapori ya akiba ya Mkungunero na Swagaswaga ikiwa ni ziara yake ya kikazi wilayani Kondoa mkoani Dodoma.

Naibu Waziri huyo alisema kuwa shutuma hizo za rushwa zitaisha tu pale watakapokamata mifugo pamoja na wachungaji wake.

Kanyasu alisema hadi sasa kuna mifugo zaidi ya 200 katika Pori la Akiba la Mkungunero pekee ambayo ilikamatwa bila kujulikana ni mali ya nani.

"Sitaki kusikia kuanzia sasa eti mmeikamata mifugo bila mchungaji au mmiliki, hakikisheni mnapiga kambi hapo hata ikiwa wiki mbili hadi pale mmiliki atakapojitokeza ili mmkamate yeye pamoja na mifugo yake," alisisitiza.

"Yaani Serikali imewagharamia kuwapa mafunzo ya kijeshi ya namna ya kupambana na wahalifu halafu unaniambia kuwa wachungaji wa mifugo hiyo mara baada ya kuwaona hukimbia kwa kupanda juu ya miti, kwanini na wewe usipande huko huko" Alihoji.

Kwa upande wake, Ofisa Wanyamapori, Raphael Ochieng, alimueleza Kanyasu kuwa mara nyingi wanapokamata mifugo hiyo wachungaji huwakimbia na kupanda juu ya miti bila wao kuwaona, hivyo huwa vigumu kuwakamata.

Aliongeza kuwa si kweli kuwa huomba rushwa wanapokamata mifugo hiyo, na kwamba hizo ni lugha za wafugaji za kutaka kuwachafua kutokana na kufanya kazi yao ya uhifadhi kwa uaminifu wa hali ya juu.

Naye Joshua Samson, askari wanyamapori, alieleza kuwa mara nyingi mifugo hiyo huchungwa na watoto wa wamiliki, na wanapowaona askari wanyamapori watoto hao hukimbia.

Alifafanua zaidi kuwa kwa kuwa kwenye hifadhi kuna vichaka na misitu mizito, huwa ni ngumu kutambua kuwa wamekimbilia wapi.

# Chadema wataka haki uchaguzi serikali za mitaa

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimewataka wasimamizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa kuusimamia vyema ili haki itendeke na kuto-rudia makosa yaliyofanyika katika uchaguzi mdogo uliofanyika katika maeneo mbalimbali nchini hivi karibuni.

Uchaguzi wa serikali za mitaa umepangwa kufanyika Oktoba katika halmashauri zote 185.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Chadema, Reginald Munisi, alidai uchaguzi mdogo wa wabunge na madiwani uliofanyika katika maeneo mbalimbali nchini hivi karibuni, ulikuwa na dosari nyingi, hivyo kuna haja wasimamizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa wakaipanga kuziepuka.

"Sisi (Chadema) tunataka haki itendeke kwenye uchaguzi huu wa serikali za mitaa, tumeona kwenye uchaguzi mdogo uliotangulia, pamekuwa na dosari nyingi, sasa zisije kujirudia.

"Tunashauri polisi na wasimamizi wa uchaguzi wasiwe chanzo cha kuvuruga uchaguzi kwa kuwa watajikuta peke yao," alisema. Munisi alisema Chadema imejipanga kufanya vizuri katika uchaguzi huo, akieleza kuwa kuna mipango na mikakati ambayo inatofautiana kulingana na eneo husika. Alisema mkakati wao wa jumla ni kuhakikisha chama hicho kinaibuka na ushindi mnono katika uchaguzi huo.

"Tuna mipango tofauti tofauti kulingana na utofauti wa kila eneo, nia yetu ni kuhakikisha tuna pata viti vingi zaidi katika serikali za vijiji na mitaa na uchaguzi wa mwaka huu utakuwa mgumu zaidi kuliko uchaguzi wowote uliowahi kutokea," Munisi alisema.

Uchaguzi wa serikali za mitaa hufanyika kila baada ya miaka mitano. Tayari serikali imeshaweka wazi kuwa kanuni mpya za kuendesha uchaguzi huo ziko tayari.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya Mwanzo ya Uyole**
**Wilaya ya.. Mbeya**
**MADAI NAMBARI...165....YA....2019**
**Mdai.....Asante Finance (Charles Mwita)**
**Mdaiwa. Fredrick Alphonce Sanga**

**Kwa Fredrick Alphonce Sanga**
**Wa Mtaa wa Chemichemi-Uyole**
**Mbeya.**
**K.K. Wito utangazwe kwenye gazeti la serikali**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta madai yake/yao kwamba**
**...Ni juu ya madai ya 7,202,000/=..........**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumanne ......tarehe 23/4/2019..saa..2:30..asubuhi/alasiri.Kwa kujibu Madai hayo na kwa kuwa hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mshauri wako /wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu ,Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Lakiri hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe..12-4-2019..

215189102



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**18 - 04 - 2019**

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe 07-04-2019 kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TUNDUMA kuelekea DAR ES SALAAM**, gari hilo lenye namba za usajili: **T 591 CHM / T 410 DDG**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 21** |
| **Upana** | - | **mita 3.00** |
| **Kimo** | - | **mita 4.6** |

3. Njia itakayotumika: TUNDUMA hadi DAR ES SALAAM kupitia VIGWAZA, Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215188702



chemicotex
the brands for you

**TAARIFA KWA UMMA**



*Zuberi Mhando*

Hii ni kutaarifu umma kwamba wenye picha hapo juu **Zuberi Mhando** si mfanyakazi tena wa Chemi & Cotex Industries LTD Tawi la Morogoro kuanzia tarehe 18-03-2019.

Tunaomba kuutangazia Umma kwamba kampuni ya Chemi & Cotex haitahusika na miamala itakayoingizwa au shughuli yoyote itajayofanywa na mtajwa hapo juu kwa jina la kampuni. **MOR/RB/4140/219**

.Utawala

115187502

# Sakaya : Hekima haikutumika shauri la CAG Assad

## ■Afichua mpango kuwashughulikia wabunge wa CUF wanaomuunga mkono Maalim Seif

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Magdalena Sakaya (pichani), amekosoa uamuzi wa Bunge kutofanya kazi na Prof. Mussa Assad, akidai kuwa hekima haikutumika kwa pande zote mbili katika kushughulikia shauri dhidi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu huyo wa Hesabu za Serikali (CAG).

Katika kikao cha kwanza cha Bunge la Bajeti Jumanne ya wiki iliyopita, Bunge lilipitisha azimio la kutofanya kazi na Prof. Assad baada ya Kamati yake ya Kudumu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kumtia hatiani kwa kutoa kauli iliyotafsiriwa kuwa ililenga kukidharau, kukidhalilisha na kukishusha heshima na hadhi chombo hicho cha kutunga sheria.

Prof. Assad alifika mbele ya kamati hiyo na kuhojiwa bungeni jijini Dodoma mwishoni mwa Januari, mwaka huu, kutokana na kauli yake ya mwanzoni mwa mwaka akiwa New-york, Marekani kwamba anafikiri "huo ni udhaifu wa Bunge".

Katika mahojiano na Nipashe mjini Dodoma juzi, Sakaya alikosoa uamuzi uliochukuliwa dhidi ya Prof. Assad, akieleza kuwa umesababisha sintofahamu ambayo kulikuwa na uwezekano wa kuiepuka kwa pande zote mbili (Bunge na Prof. Assad) kuwa na hekima wakati wa kushughulikia shauri hilo.

Mbali na sakata la CAG Assad, katika mahojiano hayo, Sakaya pia alizungumzia kuhama chama kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad na hatima ya wabunge wa CUF ambao bado wanamuunga mkono makamu wa kwanza huyo wa zamani wa Rais wa Zanzibar.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na Mbunge huyo wa Kaliua:-

**SWALI:** Bunge limeazimia kutofanya kazi na Prof. Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Una kauli ipi kuhusu uamuzi huu wa kwanza kuchukuliwa dhidi ya CAG katika historia ya Bunge la Tanzania?

**SAKAYA:** Bunge limeazimia kutofanya kazi na mtu na si Ofisi ya CAG. Limechukua uamuzi huo kutokana na kile alichokisema yeye mwenyewe, si ofisi yake iliyosema kwamba Bunge ni dhaifu.

Kilichotokea mimi naona ni kukosekana kwa hekima kwa pande zote mbili. Ndicho ninachoweza kusema kwa sababu suala la CAG kuitwa kwenye Kamati ya Maadili ya Bunge ni jambo la kawaida. Watu wengi wamewahi kuitwa.

Wapo wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi waliitwa na wakajieleza kwa kile kilichotokea wakawa huru. Wengine waliomba radhi kwa kile kilichotokea.

Sasa, kilichotokea kwa CAG ni kwamba alikataa, akisisitiza kile alichofanya si kosa, lakini ukiangalia maneno yake kuwa Bunge ni dhaifu, yana ukakasi.

Kwa maoni yangu, CAG anapoandaa taarifa zake, anazikabidhi kwa Rais na zikitoka huko zinaletwa hapa bungeni zinajadiliwa. Na Bunge limekuwa likitoa mapendekezo yake kwa serikali na kuishauri serikali hatua za kuchukua.

Sasa, wanaopaswa kufanyia kazi ripoti ya CAG si Bunge, ni serikali. Udhaifu unaoibuliwa na CAG -- kuwapo kwa ubadhirifu wa fedha za umma, fedha za halmashauri fulani zimetafunwa, udhaifu katika ukusanyaji wa mapato, vitabu feki, bajeti inavyotumika, si Bunge linalosimamia.

Kwa hiyo, serikali inaagizwa na Bunge ihakikishe upungufu wote unaoibuliwa na CAG unafanyiwa kazi. Lakini malalamiko ya CAG miaka yote, kuanzia kipindi cha (Ludovick) Utouh mpaka leo, ni kwamba taarifa zao hazifanyiwi kazi kama inavyotakiwa.

Kumekuwa na udhaifu huo wa kutofanyia kazi changamoto zinazoibuliwa. Mimi nikawa najiuliza 'tatizo kubwa ni Bunge ambalo limejadili au serikali ambayo imeshindwa kutekeleza?'

Mimi nachoona ni kwamba Bunge lina sehemu yake, lakini serikali ndiyo inatakiwa kufanyia kazi Bunge linavyoagiza. Na bahati nzuri masuala mengine tunaagiza wazi kwenye mijadala yetu ambayo inaonekana.

Kwa hiyo, udhaifu mkubwa hauko kwa Bunge, ni serikali kutokana na kutofanyia kazi mapendekezo ya Bunge. Alichokisema CAG nafikiri alipaswa kukielekeza serikalini, kwamba yanayojadiliwa na Bunge haiyafanyii kazi, lakini yeye katua mzigo wote kwa Bunge.

Na Bunge kama taasisi, lazima haitapenda kuchafuliwa. Kuna sehemu yake limefanya kwa sababu kuna mihimili tofauti hapo; Bunge na serikali.

Sisi kama wabunge tukaona kwamba Bunge halikutendwa haki, kwamba lenyewe ni dhaifu wakati wajibu wake kujadili na kutoa mapendekezo ya ripoti ya CAG imeutekeleza na tatizo limeelekezwa serikalini.

Baada ya hayo, kilichofuata sasa ni CAG kuitwa mbele ya kamati. CAG kwa kile ninachokiona ameelekeza mzigo mkubwa kwa Bunge, kitu ambacho si sahihi, angeomba tu radhi kwamba jamani nilisema hivyo kwa sababu taarifa hazifanyiwi kazi na serikali, lakini yeye akasema si kosa.

Na kwa kuwa aliulizwa kwa namna yoyote kwamba anaweza kuondoa 'statement' (kauli) yake, akakataa, hamna namna nyingine zaidi ya kuchukua uamuzi ule.

Lakini, uamuzi ule ni mkubwa sana ndiyo maana sisi kama Bunge tumebaki kwenye 'dilema' (sintofahamu). Ripoti ya CAG tayari imeshawasilishwa kwa Rais. Na kwa kuwa imeshawasilishwa na CAG huyu (Prof. Assad), inabidi iletwe hapa bungeni, lakini tayari Assad aliyeitia saini tumeingia kwenye mgogoro naye.

Tumebaki kwenye 'dilema' hiyo kwa sababu ya kitu kidogo cha ama samahani nimekosea au tukatumia hekima nyingine tofauti na ile adhabu iliyotolewa kwa sababu tulikuwa na nafasi ya kutoa adhabu nyingine na mambo mengine yakaendelea.

Kwa hiyo, nipo hapo katikati, kwamba tupo kwenye 'dilema' kwa sababu ya kukosekana kwa hekima ya kuchukua uamuzi usiokuwa na madhara makubwa kwa utendaji wa pande zote mbili.

**SWALI:** Kuondoka kwa Maalim Seif, kumeithiri vipi CUF?

**SAKAYA:** Mimi sijaona madhara yoyote ndani ya chama. Kuna kutikisika kama inavyotokea pale mwanachama yeyote anapoondoka ndani ya chama.



Mwanachama kuhamia chama kingine inaruhusiwa kikatiba. Kwa hiyo, Maalim Seif hajatenda kosa la jinai wala si kitu cha ajabu. Na kuondoka kwake ni kwa sababu ameona alichokuwa anakitafuta CUF hajakipata.

Alifungua kesi kama 35 hivi mahakamani na kesi zilizokuwa za msingi ni mbili. Mahakama ikatoa hukumu, akashindwa na akakubaliana na hukumu na akaamua kuondoka.

Kuondoka kwake hakuna madhara kwa sababu CUF ni taasisi, CUF si ya mtu. Mimi niko pale kama kiongozi, Prof. (Ibrahim) Lipumba yuko kama kiongozi aliyepewa dhamana kikatiba. Na hata Seif alikuwa kiongozi aliyepewa dhamana ya kikatiba, ameondoka, majukumu yake kapewa mwingine.

Taasisi itaendelea na lazima ifike mahali iende, haijalishi upo ama haupo. Ndiyo maana chama kikawa na katiba yake inayojitegemea.

Seif ameondoka kama ushabiki fulani hivi na wengine kufuata mkumbo, wakahamaki na kuchoma bendera, wakafanya uharibifu, wakavunjavunja mali, ofisi zetu za Zanzibar zimevunjwa, wameharibu mpaka vioo, meza, ni hujuma ambayo haikutakiwa kufanywa kabisa kwa kiongozi ambaye umekaa ndani ya chama kwa zaidi ya miaka 30.

Nafikiri hawakufanya sahihi kabisa. Kama aliamua kuhama, wangehama tu bila kufanya uharibifu. Juzi tulishuhudia Edward Lowassa anarejea tena CCM, hajafanya uharibifu wa aina yoyote. Ameikuta Chadema ikiwa pale na ameiacha ikiwa palepale.

CUF itajengwa kwa sababu CUF si Seif na Seif si CUF. Ukiwa ndani ya chama hiki, utathaminiwa kwa nafasi yako, ukiondoka, watakaokuwapo watakiendeleza. Kwa hiyo, kuondoka kwake, hakuna madhara yoyote.

Kuna viongozi tumefanya mkutano wa uchaguzi mkuu ndani ya chama wamechaguliwa kuwa viongozi wakuu wa chama na tuma viongozi hadi ngazi za chini na sasa tunajiandaa kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu ujao. Kwa hiyo, CUF kama taasisi ipo pale inaendelea kufanya kazi.

**SWALI:** Kwa haya yanayotokea ndani ya chama, matumaini ni makubwa kiasi gani kwamba CUF itaendelea kuwa na wabunge wengi hata baada ya Uchaguzi Mkuu ujao?

**SAKAYA:** Wabunge wataendelea kuwapo kwa sababu hata sasa navyoongea na wewe, wabunge ambao walikuwa wamevutwa kumfuata Seif, baada ya kuona amekwenda ACT, wengi wamerudi na wameomba kuendelea kuwapo ndani ya chama na kushiriki kufanya kazi za chama.

Hata kule Zanzibar, kuna watu ambao wanajua yaliyofanywa na CUF. Hakuna chama kilichopigania haki za Wazanzibar kama CUF chini ya kiongozi wake huyu Prof. Lipumba na Mapalala. Walipigana sana kwa ajili ya haki za Wazanzibar.

Kwa hiyo, Wazanzibar wenyewe wanajua tuliyowatendea. Hili wimbi la kuyumba na kutishwa, kutengwa, wao wanasema chama wanakijua tangu mwanzo ni CUF.

INAENDELEA UK. 26

# Madereva malori mchanga walia kamata, faini za polisi

**Na Yasmine Protace,**
MKURANGA

BAADHI ya madereva wa malori ya mchanga, ambao wanachimba madini hayo katika Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wamelalamikia Jeshi la Polisi kwa kuwakamata pasipo sababu na kuwalipisha faini.

Mbali na kulipa faini kwa kukamatwa ovyo, pia wamedai jeshi hilo limekuwa likiwabambikia makosa kuwa yanapakia mchanga usiku, wakati sheria haziruhusu.

Wakizungumza na waandishi wa habari, madereva hao walidai kuwa wanaiingizia halmashauri ya Mkuranga mapato, lakini wanasikitika kukamatwa ovyo na Polisi na kubambikiziwa kesi za kuchimba mchanga usiku na kuzidisha uzito wa mchanga kwenye magari yao.

Jumanne Rashid, dereva wa lori la mchanga ambaye anachimba Kijiji cha Dundani, alisema mchanga wanaanza kuchimba saa 12 asubuhi kama sheria zinavyowataka na kuusafirisha katika muda usiozidi saa 12 jioni.

"Pamoja na kufuata taratibu hizo, lakini polisi wanafika katika mchimbo na kutukamata wakidai mchanga tumeuchimba usiku na pia tunaambiwa magari yetu hayana rangi na kulipishwa faini ya Sh. elfu 30 kwa kosa," alisema.

Aliongeza kuwa wanafika katika mchimbo saa tisa usiku wanasubiri papambazuke, lakini polisi wamekuwa wakiwakamata wakiwa katika machimbo na kuwafungulia kesi za kuchimba mchanga usiku na kuwalipisha faini.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Filbeto Sanga, alikanusha madai hayo na kusema hakuna anayeonewa.

Alisema kutokana na ajali ya lori iliyotokea majira ya alfajiri miaka ya nyuma na kuua famili ya watu 14, serikali iliagiza malori ya mchanga mwisho kutembea saa 12 jioni ikiwamo na kuchimba mchanga asubuhi.

Alisema pamoja na katazo hilo, baadhi ya madereva wameonekana kukiuka sheria na ndio wanaokamatwa na kulipishwa faini.

"Polisi wanafanya doria maeneo mbalimbali kwa ajili ya usalama wa raia kama kazi yao inavyowaongoza," alisema Sanga na kuongeza:

"Lakini katika doria wamekamata malori ya mchanga saa tisa usiku yakiwa yanapakiwa na hivyo ndio sheria inapofuata mkondo."

Kwa mujibu wa Sanga, yapo malori ambayo yalikamatwa na mchanga umezidi na walipoyapima katika mizani yalionyesha kuzidisha uzito nayo yalilipishwa faini.

Pia Sanga alisema baadhi ya madereva walipohojiwa walikiri kuchimba mchanga usiku wa manane ili kuuwahisha kwa wateja kutoka na na mahitaji kuwa mengi.

Alisema kutoka na maelezo yao, hakuna aliyeonewa na malori zaidi ya 10 yalifikishwa polisi na kulipa faini kisha kuruhusiwa kuondoka.

Alisema pamoja na madereva hao kulipa faini, waliendelea kuyaacha malori hayo polisi na kwenda katika vyombo vya habari na kulalamika kuwa polisi imeyazuia malori yao ya mchanga katika kituo cha polisi.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa, Philemon Namwenga (wa tatu kulia), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa mnara mpya wenye uwezo wa 3G katika Kijiji cha Idete, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Meneja wa Tigo Kanda ya Kusini, Abbas Abdurahaman na wa kwanza kulia ni Diwani wa Viti Maalum Kata ya Idete, Elina Kivegele. **MPIGAPICHA WETU**

## Watalii kutoka Israel watua nchini

**Na Salome Kitomari**

ZAIDI ya watalii 1,000 kutoka Israel wamewasili nchini kwa ajili ya shughuli za utalii kwenye hifadhi za taifa, maeneo yaliyohifadhiwa, mapori ya akiba na mapori tengefu nchini kwa wiki moja.

Watalii hao waliwasili nchini kupitia uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), kwa ndege ya kwanza iliyokuwa imebeba watalii 124 ya pili 272 na ya tatu 274.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Devota Mdachi, watalii wengine 250 waliwasili juzi usiku.

Aidha, watalii hao waliwasili kwa kutumia ndege za Shirika la Ndege la EL Al zikiwa ni ndege mbili aina ya Boing 777-200 pamoja na ndege ndogo ya shirika hilo, na kwamba wengine watawasili kwa ndege ya Shirika la Ndege la Precision.

Mdachi alisema ujio wa watalii wengi ni hatua kubwa ya kujivunia kwamba ushirikiano baina ya TTB, sekta binafsi na Ubalozi wa Tanzania nchini Israel umeleta hamasa.

Alisema mafanikio hayo ni matokeo ya mikakati ya utangazaji vivutio vya utalii kulikofanywa na TTB kuanzia mwaka 2017.

# DC agawia shule, taasisi sukari ya magendo

**Na Robert Temaliilwa,**
BAGAMOYO

MKUU wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Kawawa, amegawa sukari mifuko 227 yenye ujazo wa kilo 50 kila mmoja ambayo iliingizwa katika wilaya hiyo kwa njia za magendo.

Akikabidhi sukari hiyo kwa wakuu wa shule na wakuu wa vituo vya kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu, Kawawa aliwaonya wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa zao wilayani hapa kupitia bandari bubu.

Alisema kamati yake ya ulinzi na usalama ya wilaya imejipanga kuhakikisha wanadhibiti mianya ya wafanyabiashara wanaokwepa kulipa ushuru wa serikali.

Kawawa alisema amefanya juhudi ya kusimamia idara zinazohusika kurahisisha masharti ya uingizaji bidhaa katika bandari ya Bagamoyo, hivyo wafanyabiashara hawana sababu ya kupitisha bidhaa zao kwa njia za magendo.

Alifafanua kuwa ameitisha kikao cha wafanyabiashara pamoja na idara za serikali ili kuondoa urasimu wa vibali vya kuingiza bidhaa ikiwa ni njia ya kuwasaidia wafanyabiashara hao wasikwepe ushuru wa serikali.

Alizitaja idara ambazo amezikutanisha na wafanyabiashara hao ni Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Mamlaka ya Mapato (TRA), Mamlaka ya Bandari (TPA), Idara ya Forodha na Ushuru wa bidhaa, pamoja na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Kawawa alisema lengo la kikao hicho cha pamoja lilikuwa ni kutoa maelekezo nafuu yatakayowawezesha kutumia bandari halali ya Bagamoyo ili serikali iingize mapato kupitia bidhaa zinazoingia katika wilaya hiyo.

"Nimewakutanisha wafanyabiashara wote wanaoingiza bidhaa katika wilaya yangu na TFDA, TRA, TPA watu wa idara ya Forodha ili kutengeneza mazingira mazuri kwa wafanyabiashara, hivyo sitarajii baada ya hapo kuwapo na wafanyabiashara wanaokwepa ushuru wa serikali, " alisema.

Aliongeza kwa kuwaonya wale wote aliowagawia sukari hiyo kuitumia kwa mujibu wa maelekezo yake na wala wasiitumie kwa manufaa yao binafsi.

Alisema endapo atabaini kuna mtu ametumia sukari hiyo kinyume cha utaratibu atamchukulia hatua za kinidhamu.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Ushauri wa maaskofu sasa ufanyiwe kazi*

**MAASKOFU** wa madhehebu mbalimbali ya kikristo wamebainisha mambo mbalimbali ambayo kwa namna moja ama nyingine yanakwaza maendeleo katika jamii.

Waliyazungumza hayo wakati wa ibada za sikukuu ya Pasaka ikiwa ni kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo zaidi ya miaka 2000 iliyopita.

Miongoni mwa mambo hayo ni kutaka viongozi wenye mamlaka kutenda haki ili kuepisha mifarakano ambayo inaweza kutokea katika uchaguzi wa serikali za mitaa ambao unatarajiwa kufanyika mwaka huu, kutaka kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya rushwa miongoni mwa watumishi wa umma, kazi kubwa ya kuvunjika kwa ndoa za kikiristo na riba kubwa za mikopo inayotolewa na mabenki.

Viongozi hao pia waligusia masuala ya umuhimu wa huduma nzuri ya bima ya afya kwa Watanzania wote pamoja na uboreshaji zaidi wa kiwango cha elimu elimu.

Mmoja wa maaskofu aliwataka viongozi wanaosimamia haki nchini kutimiza wajibu wao ili kuepusha taifa kuingia katika mifarakano itakayo sababisha viasharia vya uvunjifu wa amani na kulikosesha taifa utulivu wa amani.

Alisema taifa limebahatika kupata viongozi waadilifu ambao wameendelea kudumisha amani kwa kutenda haki, hivyo wasijitokeze wachache ambao watataka kuonyesha nguvu ya nafasi zao katika kuliongoza taifa kwa kutaka kufarakanisha jamii kwa sababu ya maslahi yao

Kwamba mifarakano ambayo imekuwa ikijitokeza nchini na katika nchi kadhaa mara kadhaa imekuwa ikisababishwa na viongozi wachache wanaosimamia haki kupitia nafasi zao, ambao wamekosa uadilifu wa kusimamia haki.

Alisema hivi karibu taifa litaingia katika uchaguzi wa serikali wa mitaa ambao ndio msingi wa uchaguzi mkuu wa 2020, hivyo aliomba uchaguzi huo uwe wa haki na asitokee kiongozi yeyote mwenye mamlaka akapindisha haki.

Aliongeza kama uchaguzi wa serikali za mitaa usipofanyika kwa haki na uhuru, hata uchaguzi mkuu unaweza ukavurugika.

Moja ya makanisa, limeiomba serikali kuweka mikakati madhubuti ya kifedha na utaratibu wa kuchangia bima afya kwa watu ambao hawana uwezo wa kupata huduma hiyo waweze kuipata, likisema kuna idadi kubwa ya Watanzania ambao ni maskini na wameshindwa kupata huduma hiyo.

Kuhusu elimu, imeelezwa kubadilishwa kwa sera na miongozo ya elimu ni ishara ya wazi kwamba Watanzania bado hawajui wanachokitaka, na kwamba sekta hiyo bado kama taifa halijajua rasilimali watu wawe na sifa gani, hawajui wanataka taifa la leo na kesho liweje.

Aidha, mikopo inayotolewa na mabenki imelalamikiwa kuwa riba yake ni kubwa, hivyo haiwezi kuwanufaisha maskini hususan makundi ya vijana.

Mmoja wa maaskofu alishangazwa na kasi ya kuvunjika ndoa za kikristo na kuwa kanisa linajiuliza ni kwa nini nyingi zinavunjika kuliko wakati mwingine wowote, huku akieleza chanzo ni watu kushindwa kuzingatia ahadi na mapatano waliyowekeana mbele za Mungu.

Ni imani yetu kuwa ushauri uliotolewa kwa serikali kuhusiana na changamoto hizo itakuwa imesikia na itazingatia ushauri huo na kuufanyika kazi kwa nia nzuri ya kujenga.

Kwa yanayoihusu jamii bila shaka kila mmoja atakuwa amesikia na atachukua hatua stahiki.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

# *Teknolojia rahisi itaongeza tija katika sekta ya kilimo*

**KILIMO** ndiyo sekta ambayo inaajiri takribani asilimia 70 ya Watanzania, takribani milioni 55 kwa hivi sasa, wengi wakiishi vijijini kwa mujibu wa takwimu kutoka vyanzo mbalimbali nchini.

Hata hivyo, karibu asilimia 70 ya wakulima hawa ambao ndio tegemeo kubwa katika suala zima la usalama wa chakula ngazi ya kaya na taifa kwa ujumla, ni wakulima wadogowadogo, ambao hujishughulisha na kilimo kati ya nusu ekari hadi ekari tatu kwa ujumla.

Asilimia 70 ya wakulima hawa wadogo ni wanawake na ndiyo wanaotegemewa kuzalisha chakula katika ngazi ya kaya ya kulisha wananchi wengine kwenye majiji na miji mbalimbali nchini, licha ya kutoa malighafi kwa Tanzania ya viwanda.

Kwa muda mrefu sasa maisha ya wakulima hawa yameendelea kuwa duni kutokana na nguvu zao wanazowekeza katika kilimo, kutokuwa na tija ya kuonekana kwenye uzalishaji wa kile wanacholima.

Hali hiyo inatokana na sababu mbalimbali, baadhi ikiwa uduni wa zama wanazotumia.

Hadi sasa bado wakulima wadogo wanatumia jembe la mkono ambalo ni la toka enzi na enzi katika mnyororo mzima wa kilimo, yaani kulima na palizi.

Bado wanatumia njia za kiasili ama za kienyeji kupanda mazao shambani ambazo kimsingi hazitoi fursa ya kupata mazao mengi.

Wanatumia njia za kienyeji katika uvunaji wa mazao yao na kuyahifadhi, hali inayosababisha wakati mwingine yaharibike.

Hawapati huduma za ughani kama vile mbolea, ushauri wa wataalamu kwenye mlolongo mzima wa kilimo kuanzia namna ya kupanda mazao, mambo ya kuzingatia, matumizi ya dawa za kuua wadudu na hata katika eneo la uvunaji na uhifadhi.

Wameshindwa kuwa na tija kwenye uzalishaji kwa sababu ya serikali na wadau kutowekeza katika maeneo ambayo yana tija ya moja kwa moja kwao.

Na ndiyo maana inapotokea kwa mfano mvua ikakosekana kipindi cha masika ama vuli shida huingia kwa sababu mazao hukauka, suala ambalo lisingetokea iwapo wangewezeshwa katika teknolojia ya umwagiliaji.

Hata hivyo, kuna eneo jingine ambalo kama lingetiliwa mkazo kwa kuwekezwa rasilimali za kutosha, lingeweza kuwa mkombozi kwa wakulima wetu.

Eneo hili ni la ubunifu wa mashine rahisi na zenye gharama nafuu maalumu kwa ajili yao.

Na ndiyo maana Muungwana anaona wakati umefika sasa kwa serikali na wadau wengine wa kilimo kutupia jicho eneo hili kwa kugharimia ubunifu wa mashine ndogo na rahisi ili kuongeza tija katika sekta ya kilimo.

Wakulima wadogo wanahitaji majembe rahisi yayoliboreshwa ambayo yatachukua nafasi ya jembe la mkono.

Wanahitaji mashine za kupandia zitakazowawezesha walau kupanda ekari moja kwa siku.

Aidha, wanahitaji pia mashine za kunyunyizia dawa, za kuvunia pamoja na teknolojia rahisi ya kuhifadhi mazao yao.

Hili linawezekana kama kipaumbele kitatolewa kwenye eneo hili na serikali pamoja na wadau kama mashirika yasiyo ya kiserikali.

Muungwana hatoi wito kwa mashirika yasiyo ya kiserikali tu, bali hata kwa serikali kupitia taasisi zake za kitaalamu ambazo zinaweza kabisa kuwekeza katika teknolojia rahisi ya kusaidia wakulima.

Taasisi kama ile ya Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), taasisi za teknolojia ama vyuo vikuu ambavyo vina idara za uhandisi.

Hivyo basi ni wakati sasa wa kusaidia sekta ya kilimo kupitia uwekezaji katika teknolojia za mashine rahisi zitakazosaidia wakulima wadogo wazalishe kwa tija.

Hili linawezekana kabisa kwa kutenga bajeti maalumu kwa ajili ya kufanya kazi hii, ambayo ina faida kwa kundi kubwa la Watanzania na matunda yake yanaweza kabisa kuwavutia vijana wakaingia kwenye sekta hii kwa nguvu zote na hivyo kupunguza tatizo la ajira nchini.

# BARUA/MJADALA

## Taaluma hii itendewe haki

**Mhariri,**

*NIPATIE fursa ya kuzungumzia kidogo ninachoona ni tatizo kwa baadhi ya watangazaji wa redio na televisheni, pale wanapokuwa wanajadili ama kuongoza mada iliyoko mezani katika baadhi ya vituo vya televisheni na redio.*

*Kilichonivuta niweke hili suala kwako, ni baada ya kumsikia mtangazaji mmoja aliyekuwa akisoma taarifa mbalimbali zilizoandikwa magazetini, akishangaa kwa nini mikopo kwa ajili ya masomo ya elimu ya juu inayotolewa na bodi wanapewa pia wanafunzi wanaosoma kwenye vyuo vya elimu ya juu, vinavyomilikiwa na watu binafsi.*

*Nilivyomuelewa mimi, mtangazaji huyo alikuwa anamaanisha kwa ufahamu wake kuwa, mikopo kwa ajili ya kusoma vyuo vya elimu ya juu nchini ni maalumu kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya umma tu.*

*Nimeamua kusema hili baada ya kung'amua kuwa, baadhi ya watangazaji wetu kwenye baadhi ya redio na televisheni nchini wanakuwa hawana ufahamu wa kutosha wakati mwingine kuhusiana na wanachochangia kwenye baadhi ya mada wanazoziendesha.*

*Ninaomba kupitia kwako mhariri, kwa baadhi ya vituo vya redio na televisheni zikaona umuhimu wa kuweka watu wenye ufahamu wa kutosha kwenye mada zinazowasilishwa mezani, ama wanapochangia kwenye habari na makala zilizoandikwa magazetini.*

**Mpenda ukweli, Dar es Salaam**

## Serikali itatue kero hii

**Mhariri**

*NINAJITOKEZA katika ukurasa wako wa maoni ili niweze kueleza kero ya muda mrefu inayotupata sisi wakazi wa Maramba Mawili, Wilaya mpya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam.*

*Kero ninayoieleza kwa leo ni ya ukosefu wa huduma ya uhakika ya maji ya bomba katika eneo letu, tofauti na ilivyo katika maeneo mengine ya jiji hili.*

*Kwa muda mrefu tumeahidiwa na serikali yetu kupatiwa huduma hiyo ya maji ya bomba ambayo kimsingi ndiyo huduma ya uhakika zaidi, ikilinganishwa na vyanzo vingine kama ya maji ya visima.*


*Ninaomba kupitia kwako Mhariri kwa serikali na hasa walio na mamlaka katika sekta ya maji, wasikie kilio chetu cha muda mrefu, na hatimaye watuletee huduma hii muhimu kwa maisha ya binadamu.*

**Muathirika, Dar**

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# 'Mahakama za wazi' ni muhimu lakini zizingatie sheria za nchi




**Na Salome Kitomari**

KUMEKUWA na utaratibu wa baadhi ya viongozi wa serikali kusikiliza kero za wananchi kwenye mikutano ya hadhara na kutoa uamuzi au maelekezo yenye 'utata' katika siku za hivi karibuni.

Kwamba baada ya kumaliza kuhutubia, viongozi hutoa fursa kwa wananchi wenye kero ili wazitatue lakini pia maoni kwa ajili ya kuyafanyia kazi.

Mjadala unaona kwamba huu ni utaratibu mzuri kwani huwezesha utatuzi wa baadhi ya changamoto zilizopo, lakini pia unawafanya wananchi wajione wamesikilizwa na viongozi wao.

Kimsingi zipo changamoto za wananchi zinazoweza kutatuliwa kwa haraka kupitia utaratibu huu, kwani hazihitaji kufuata utaratibu wowote wa kisheria.

Kwamba kama ni tatizo lililokwama kushughulikiwa kwa muda mrefu na mtumishi wa umma aliye chini ya mamlaka ya kiongozi anayehutubia wananchi, basi ni suala la kutoa maelekezo na utekelezaji ukafanyika mara moja.

Hata hivyo, kupitia mitandao ya kijamii tumeona jinsi baadhi ya viongozi wanavyoshughulikia kero mbalimbali za wananchi, lakini wakivuka mpaka wakati mwingine na kuingilia masuala ya kisheria.

Nasema ya kisheria kwa maana kuwa yanahitaji mchakato maalumu katika utekelezaji wake, hali inayofanya watumishi wa umma wanaopewa maelekezo kuyatekeleza kwa shinikizo.

Mathalani, ipo baadhi ya mikoa iliyo na 'Mahakama za wazi.'

Kwamba kiongozi kama Mkuu wa Mkoa (RC) au Wilaya (DC) anaelezwa kero ya mwananchi ambayo iko mahakamani, lakini bado akataka aingilie uhuru wa Mahakama.

Kwamba ikiwa DC au RC kalalamikiwa na mwananchi, anaagiza Mahakama ifikishe jalida la kesi husika ofisini kwake katika kipindi cha siku moja au mbili, wakati anajua kuna taratibu za kufuata ili kupata jalada la kesi iliyoko mahakamani.

Mifano ipo ya kiongozi anaamrisha watafsiri sheria kufanya jambo fulani kwa mwananchi bila kuangalia katika shauri husika kuna pande mbili zinazovutana na wakati mwingine kinachoangaliwa na Mahakama ni ushahidi uliowasilishwa.

Kuna mifano pia ya baadhi ya viongozi kuagiza wananchi kwenda mahakamani kudai faili la kesi iliyoamualiwa mwaka 1992, katika Mahakama ya Mwanzo.

Ni wazi katika hali hii kwa maoni ya mjadala kuwa mazingira yake tu yanaonyesha ni ngumu kupata faili husika kutokana na utunzaji duni wa kumbukumbu.

Haishangazi kukuta mafaili ya toka kipindi hicho kwenye Mahakama hiyo yamelishaliwa na mchwa, hata kama mwananchi husika katumwa au kiongozi kasikika jukwaani akitoa maelekezo kwa Mahakama kufikisha faili hilo mezani kwake ndani ya siku mbili.

Kama haitoshi baadhi ya viongozi bila kutambua umuhimu, nguvu na uhuru wa mhimili kama Mahakama, hutoa maelekezo ya kutaka kesi fulani ziamuliwe kwa haraka, wakisahau kuwa ili uamuzi wa kesi husika ufanyike ni lazima taratibu za kimahakama zifuatwe.

Kwa msingi huo, wananchi huenda kwa 'kiburi' kwa watumishi wa umma na kudai nyaraka ambazo wakati mwingine zina mchakato wake wa upatikanaji.

Huenda kwa watumishi wakijiamini na lugha zisizostahili kwa kuwa wamepewa nguvu pengine na RC au DC.

Kuna wakati yaliibuka malalamiko ambayo rais aliyatolea ufafanuzi na maelekezo kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya ma-RC na ma-DC kuwaweka ndani watu bila kuwafikisha mahakamani wakitumia sheria inayowapa nguvu ya kufanya hivyo.

Baada ya maelekezo ya rais na waziri mwenye dhamana, matukio hayo yamepungua kama si kwisha kabisa.

Sasa 'kashikashi' za viongozi wetu hao yaani ma-RC na ma-DC zimebaki kwa watumishi wa umma ambao kwa kuwa hawawezi kutoka mbele ya umma na kusema, wanajikuta katika mazingira magumu ya kutekeleza majukumu yao, hali inayoofisha wakati mwingine motisha ya kufanya kazi.

Ni kweli kuwa wapo watumishi wasiotekeleza wajibu wao ipasavyo, lakini ni vyema kusiwe na shinikizo linaloweza likaharibu utawala wa sheria kwa ujumla.

Ni kweli kwamba kuna malalamiko dhidi ya Mahakama kutokana na baadhi ya watumishi wake wasio waaminifu ambao hudai rushwa ili mtu apate haki yake.

Hata hivyo, yote hayo hayawapi nguvu viongozi kushughulikia matatizo ya wananchi yaliyokwishafikishwa mahakamani nje ya sheria.

Na pale viongozi wanapogundua uzembe au udhaifu wa utendaji kutokana na malalamiko ya wananchi katika mikutano ya hadhara, mjadala unaona ni vyema kutumia taratibu za kikazi kumwajibisha mtumishi anayebainika kutenda isivyo.

## KABWELA — NA FADHIL MOHAMMED



# Mbinu mpya za wahamiaji kuingia nchini zabainika

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani hapa mkoani Shinyanga, imesema kuwa wahamiaji haramu wanaoingia nchini kutoka nchi jirani wameanza kutumia njia mpya ya kutembea na watoto wachanga mgongoni kwa lengo la kuonewa huruma na polisi wanapokamatwa.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha. Aliyasema hayo wakati akitoa hotuba yake kwa madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Kahama katika kikao cha kawaida cha baraza la madiwani mwishoni mwa wiki kwa lengo la kujadili shughuli mbalimbali za kimaendeleo kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita.

Alisema kuwa wahamiaji hao kwa sasa wanatumia mbinu nyingine ya kutembea na watoto wachanga ili wanapotiwa nguvuni na vyombo vya dola wasamehewe kwa kuwa wana watoto hao wachanga wakidai kuwa ni wao.

Akizungumzia kuhusu masuala ya sekta ya elimu, alisema masuala ya mimba mashuleni yamekuwa yakizidi kuongezeka kila mwaka kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo walimu wenyewe na wananchi ambao wazunguka maeneo ya shule husika kuficha siri.

Alisema kuwa kwa kipindi cha mwaka 2018 jumla ya mimba za wanafunzi wa shule za sekondari katika Wilaya ya Kahama zilikuwa 21, huku kwa kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2019 wanafunzi wa sekondari 26 wameishapata ujauzito.

Nae Diwani wa Viti Maalumu kutoka katika Kata ya Malunga katika Halmashauri hiyo, Bernadetha Mbagale, alisema katika kipindi cha mwaka jana wanafunzi waliofaulu kuingia kidato cha kwanza walikuwa wengi, lakini walifaulu kwa alama ndogo wastani wa madaraja B na C walikuwa wengi zaidi na kusababisha kuwapo changamoto ya madarsa.

Mbagale alisema jitihada zinahitajika katika kuongeza ufaulu katika shule za Mingi katika Halmashauri ya Mji wa Kahama na kubaki na daraja A au B tofauti na hali iliyokuwapo katika kipindi cha mwaka jana ya wanafunzi wengi walifaulu chini ya daraja B na C.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, alisema wanafunzi wanafunzi wanashindwa kufaulu kwa kiwango cha juu kutokana na shule nyingi katika kata zao kutotoa chakula cha mchana kwa wanafunzi.



Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo (katikati) na watu wengine wakisafri kwa boti juzi kwenda kwenye kisiwa cha Rukuba jimboni humo kwa ajili ya uzinduzi wa maktaba ya Shule ya Msingi Rukuba na pia sherehe za sikukuu ya Pasaka. **PICHA: NA MPIGA PICHA WETU.**

# Waitara awageukia wanaolibeza jimbo lake

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Jimbo la Ukonga, Mwita Waitara, amesema cheo cha unaibu waziri alicho nacho hakimaanishi kuwa jimbo lake haliwezi kukosa changamoto kama inavyotafsiriwa na baadhi ya watu.

Waitara ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kwamba anatambua kuna changamoto za miundombinu katika jimbo hilo.

"Wapo ambao wanasema licha ya kwamba nimekuwa naibu waziri, nimeshindwa kutatua changamoto za jimbo, unaibu waziri hauna maana kwamba nitautumia kumaliza matatizo ya jimbo, fedha zinatolewa kwa utaratibu wa serikali," alisema.

Aliongeza kuwa haimaanishi kuwa fedha zinamiminika, lazima kuwapo na bajeti. "Ninapopata fedha za jimbo Sh. milioni 71 kila mwaka nina hakikisha zinakwenda kwenye kata na hakuna kata ambayo imekosa fedha hizo."

Alisema jimbo lina changamoto nyingi alizozikuta na tangu ameingia madarakani amejitahidi kuzipunguza ingawa bado zipo nyingine anaendelea kuzitatua.

Aidha, Waitara alisema wamejenga hospitali ya mama na mtoto katika eneo la Chanika lililogharimu zaidi ya Sh. bilion 8.4 ambalo litasaidia mama anapopata tatizo la kujifungua kupelekwa moja kwa moja katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

"Tumeshajenga zahanati nne, tumeshapeleka zaidi ya Sh. milioni 100 ambazo zimeshakamilika na kwa sasa tunajenga kituo cha afya cha Mzinga kwa Sh. 193 na mkandarasi yupo eneo la ujenzi," alisema.

Aliongeza kuwa ifikapo Juni 30, mwaka huu watakabidhiwa majengo saba na tayari wameshapatiwa Sh. bilioni 4.4.

Alisema watajenga hospitali ya wilaya na wananchi watakuwa wanatabiwa katika jimbo lao kutokana na huduma ya afya zilivyoboreshwa na kuwa za kisasa.

Aidha, alisema katika elimu mwaka huu wameandikisha watoto 17,000 na manispaa imejitahidi kutatua changamoto zilizojitokeza ili kuhakikisha wanafunzi hao wanasoma katika mazingira bora.

Waitara alisema wamejenga shule mpya za msingi tano ambazo zimeanza kazi, vyumba vya madarasa 34, ujenzi wa matundu ya vyoo 146 na kutengeneza madawati zaidi ya 6,000 ambayo yatasambazwa katika kila kata.

Alisema anajua kuna changamoto ya walimu wa Sayansi na wanakwenda kulitatua ili shule ziweze kuongeza ufaulu.

Aidha, alisema jimbo la Ukonga limepatiwa bajeti kubwa ya barabara kuliko majimbo mengine ya Manispaa ya Ilala na kwamba barabara ya Kitunda Msongola ambayo ina ukubwa wa kilometa 3.2 itajengwa kwa kiwango cha lami na baadaye zitaongezwa kilometa nne.

Alisema kinachosubiriwa na mkandarasi apatikane ili ujenzi uanze.

# CAG Assad abaini kufichwa maslahi, mikopo ya vigogo

INATOKA UK. 2

ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma Na. 20 ili kuwe na uwazi na kuaminika kwa taarifa za fedha za halmashauri," Prof. Assad anashauri katika ripoti yake hiyo.

UPEO MDOGO WA WAHASIBU

Katika ripoti yake hiyo, Prof. Assad pia anaeleza kuwa amebaini kuwapo kwa wahasibu wasio na upeo mkubwa wa kuandaa taarifa za fedha katika baadhi ya halmashauri nchini.

Anabainisha kuwa baada ya kukamilika kwa taarifa za fedha, agizo 31(1) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linamtaka ofisa masuuli kuwasilisha taarifa hizo kwa CAG kwa ajili ya ukaguzi ifikapo Septemba 30, kila mwaka.

Vilevile, mtaalamu huyo wa ukaguzi wa hesabu anabainisha kuwa Kifungu Na 45(4) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 (Iliyorekebishwa mwaka 2000), kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuziwasilisha taarifa za fedha kwa CAG mapema iwezekanavyo baada ya kufunga mwaka wa fedha.

"Kinyume cha sheria tajwa hapo juu, wakati wa ukaguzi wa taarifa za fedha za mamlaka za serikali za mitaa 185, nimebaini baadhi ya taarifa hizo zina makosa kadhaa ya kitarakimu na nyingine kuacha kuonyesha baadhi ya taarifa muhimu.

"Hii inaashiria kuwa taarifa hizo ziliandaliwa na wahasibu ambao hawana upeo wa kutosha katika kuandaa taarifa za fedha kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma.

"Nilibaini halmashauri tano zilipata hoja mbalimbali za ukaguzi zinazohusiana na makosa katika taarifa za fedha zenye jumla ya Sh. 154,626,259,685 ambazo zimenipelekea kutoa hati isiyoridhisha moja na hati zenye shaka nne," CAG Assad anabainisha katika ripoti yake hiyo.

Anapendekeza mafunzo ya mara kwa mara ya kujenga uwezo kwa watumishi yanahitajika ili kuwawezesha kuandaa taarifa za fedha zinazoendana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma na hivyo kupunguza makosa na dosari nyingine katika kuandaa taarifa za fedha.

"Maofisa masuhuli wote wa halmashauri husika pia wanapaswa kuimarisha mchakato wa kudhibiti ubora wa taarifa na kuandaa ratiba ya uandaaji wa taarifa za fedha ili kuhakikisha usahihi wa taarifa zinazowasilishwa kwa ukaguzi kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vinavyokubalika," CAG Assad anashauri.

# Malasusa atahadharisha mawakala wapinga kila kitu

**Na Elizabeth Zaya**

ASKOFU wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Alex Malasusa, amewataka Watanzania kuwa vyombo vya matumaini badala ya kuwa mawakala wa kukatisha watu tamaa na kupenda kukosoa kila jambo linalofanyika.

Dk. Malasusa alitoa kauli hiyo wakati akihubiri katika ibada ya Pasaka katika Kanisa la KKKT, Azania Front jijini Dar es Salaam juzi.

"Wako ambao wanafanyika kuwa mawakala wa kukatisha watu tamaa, kila linalofanyika hata kama ni nzuri, lakini hutafuta neno la kukatisha tamaa, iwe nyumbani katika familia, kanisani, katika vikundi vyetu na iwe katika taifa letu, lolote linalofanyika wamekuwa ni wa kukatisha tamaa," alisema Dk. Malasusa.

"Ni vema tubadilike na tufanyike vyombo vya kuleta matumaini katika jamii, tuonyeshe watu mambo mazuri, wapo watu wanaozungumzia mambo mabaya tu na hata kusambaza mambo mabaya tu na kwa nini tuendelee kuwa mawakala wa kusambaza hayo mambo mabaya tu?" alihoji Dk. Malasusa.

Alisema ni vema watu kuepuka tabia za kuona mapungufu pekee na kuyasambaza badala yake kuhubiri mema.

Aliwaomba Wakristo na Watanzania wengine kuwasaidia vijana ambao wameingia katika dawa za kulevya na kuwarudisha katika hali yao ya awali kwa kuwahubiria mambo mema. "Hata wale walioumia katika maisha yao ya ukahaba, walevi, watoaji nafsi za watu, tuwahubirie mambo mema, tuwaambie kwamba yupo Mungu ambaye anaweza kubadilisha, ni lazima tubadilike. Sisi tufanyike kuwa mawakala wa habari njema, kuishi na kuonyesha upendo katika jamii na familia," alisema Dk. Malasusa.

Aliongeza: "Wapo watu wengi ambao wako katika matatizo, tunapaswa kuwaonyesha upendo kwa kuwasaidia kuyaondoa. Tuwe watu wa amani, tusiwe watu wa kukimbilia kuiondoa amani kuanzia katika ngazi ya familia hata katika nchi yetu."



Mkuu wa Wilaya ya Ilemele, Dk. Severine Lalika (kushoto), akipokea moja ya kompyuta 10 kutoka kwa Meneja wa Kiwanda cha bia cha TBL Mwanza, Patel Kilovele, zilizotolewa na kampuni kwa ajili ya shule za msingi na sekondari za kata ya Pasiansi jijini Mwanza, na printa tatu kwa ajili ya Kituo cha Kulelea Watoto wanaoishi katika mazingira magumu cha KKKT Misungwi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vyama 7 vya upinzani kususia uchaguzi mdogo

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

UMOJA wa vyama vya siasa vya upinzani mkoani Katavi umemwandikia barua msimamizi wa uchaguzi mdogo wa udiwani wa Kata ya Uwanja wa Ndege, Manispaa ya Mpanda mkoani humo, ukidai kutoshiriki uchaguzi huo.

Vyama hivyo ADC, NCCR-Mageuzi, Chadema, ACT- Wazalendo, TLP, UDP na UMD, vilifikia uamuzi huo baada ya kikao chao kujadili kujitoa kushiriki uchaguzi huo.

Uamuzi wa vyama hivyo saba vya upinzani ulifikiwa mwishoni mwa wiki baada ya kikao chao cha pamoja kilichofanyika katika ofisi za Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) mkoa.

Katibu wa umoja wa vyama hivyo mkoani Katavi, Joseph Mona, akizungumza kwa niaba ya vyama hivyo mbele ya waandishi wa habari alisema, umoja huo umekubaliana kutoshiriki uchaguzi huo kutokana na vyama hivyo kutokuwa na imani na Tume ya Uchaguzi, kukosekana kwa takwimu ya wapigakura katika kata husika na daftari la wapigakura kutoboreshwa mpaka sasa.

Alitaja sababu nyingine kuwa ni chaguzi nyingi ndogo zimekuwa zikighubikwa na uvunjifu wa amani na kukosekana kwa haki.

Alisema vyama hivyo havitakuwa tayari kumuunga mkono mgombea yeyote wa chama cha siasa cha upinzani ambaye hayuko katika umoja huo ambaye atagombea nafasi ya udiwani kupitia chama chake.

Uchaguzi huo mdogo umepangwa kufanyika Mei 19, kujaza nafasi ya udiwani wa kata hiyo, baada ya aliyekuwa diwani wake, Stephano Asalile, kufariki dunia miezi miwili iliyopita kwa ajali ya pikipiki.

Kata nyingine ya Itenka katika Halmashauri ya Nsimbo pia ipo wazi kufuatia aliyekuwa diwani wa kata hiyo kupitia Chadema kutangaza kujivua uanachama na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

# DC awavaa wanaogushi vitambulisho

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Wialaya ya Kahama, Anamringi Macha amesema atawachukulia hatua za kisheria na kuwafikisha mahakamani baadhi wafanyabiashara wanaoghushi vitambulisho vya wajasirimali wadogo na wanaochukua vitambulisho hivyo bila kuwa na sifa.

Alisema mpaka sasa wameshakamata watu wawili ambao wanajishughulisha na kazi ya kughushi vitambusho hivyo, na wako mbioni kuwachukulia hatua za kisheria kwa kuwa ni kosa kughushi nyaraka za Serikali.

Macha aliyasema hayo katika kikao cha kawaida cha baraza la madiwani cha Halmashauri ya Mji wa Kahama mwishoni mwa wiki na kusema kuwa kitendo cha kughushi nyaraka ya serikali ni kosa na ni hatua ya ukwepaji kodi ya serikali.

Macha alisema katika siku tatu ambazo alizitumia kuwahimiza wakazi wa Halmashauri ya Mji ambao wanafanya biashara ndogo kujiandikisha kuchukua vitambulisho vya ujasirimali, wamefanikiwa kuuza jumla ya vitambulisho 2,500 vyenye thamani zaidi ya Sh. milioni 50.

"Kuna watu ambao mpaka sasa wanakimbilia kujiandikisha kupata vitambulisho hivyo kwa lengo la kukwepa kodi ya serikali na ushuru wa Halmashauri, jambo ambalo siyo sahihi kwa kuwa wanapaswa kuwajibika katika sehemu husika. Nitawachukulia hatua wale wote watakaoendelea kubainika kughushi hivyo vitambulisho," alisema.

Hata hivyo, Macha aliwataka madiwani wa Halmashauri hiyo kuendelea kuwahamasisha wananchi wao kuchukua vitambulisho vya wajasirimali wadogo kwa sababu yeye kwa muda mfupi wa siku tatu aliotumia kuwahamasisha wananchi alifanikiwa kuuza vitambulisho 2,500.

Pia amewataka wajasirimali kuvaa vitambulisho hivyo muda wote wa biashara kwa kuwa kwa sasa asilimia kubwa ya wananchi wamekuwa wakinunua bidhaa kwa wafanyabiashara wadogo wenye vitambulisho shingoni.



Muasisi wa Taasisi ya Wanasayansi Chipukizi nchini (TST), Dk. Gosbert Kamugisha (kulia), akizungumza kwenye hafla jijini Dar es salaam ya kutangaza mwaliko kwa wanafunzi wa shule za sekondari wanaofanya utafiti wa kisayansi na tekinolojia kuwasilisha maombi na maelezo ya utafiti wao kwa YST. Wa kwanza (kushoto) ni Meneja Uhusiano wa Shell, Patricia Mhondo na (katikati) ni muasisi mwenza, Joseph Clowry. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chipukizi wenye vipaji vya ugunduzi kusaidiwa

**Na Mwandishi Wetu**

VIJANA chipukizi nchini wametangaziwa fursa, baada ya kampuni ya mafuta ya Shell kuahidi kuendelea kusaidia juhudi za kukuza vipaji vya utafiti za kisayansi na ugunduzi wa teknolojia unaofanywa na vijana hao nchini.

Alizungumza kwanye hafla ya maandalizi ya maonyesho ya wanasayansi chipukizi ya mwaka huu yanayosimamiwa na Taasisi ya Wanasayansu Chipukizi Tanzania (YST) jijini Dar es Salaam, Meneja Uhushiano wa Shell, Patricia Mhondo, ndiye aliyetoa ahadi hiyo akisema kampuni yao inazipa uzito juhudi za taasisi zinazochoea tafitia na ugunduzi, na kwamba itaendelea kushirikiana kwa dhati na YST na watu binafsi zinazolenga maeneo hayo na kukuza vipaji vya utafiti wa kisayansi.

"Juhudi ya YST inakuza vipaji vya utafiti za kisayansi na ugunduzi wa teknolojia unaofanywa na vijana wadogo wa Tanzania na kuwafanya wajiamini. Aidha, juhudi hiyo inawafanya vijana wapende masomo ya sayansi, na imeifanya Tanzania ijulikane kimataifa katika nyanja za utafiti na ugunduzi. Shell itaendelea kushirikiana na YST," aliahidi.

Kadhalika, Mhondo alifafanua kuwa miradi ya vijana ambayo imechochewa na YST kutokana na maonyesho, imebadilika na kuwa miradi mizuri ya biashara.

Ahadi ya aina hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Karimjee Jivanjee Foundation (KJF), Yusuf Karimjee, na kuieleza hafla hiyo kwamba KJF itaendelea kutekeleza ahadi iliyotoa mwaka jana ya kuisaidia kifedha YST kwa kutoa dola 100,000 kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano.

"KJF imekuwa mfadhili wa YSF toka mwaka 2012," alisema Karimjee. Mmoja wa waasisi wa YST, Dk. Gosbert Kamugisha, alisema wanafunzi 200 wenye utafiti wenye viwango bora watachaguliwa kushiriki maonyesho ya YST 2019 yatakayofanyika jijini Dar es Salaam kati ya Julai 31 na Agosti Mosi, 2019. "Wanasayansi chipukizi watakofanya ugunduzi mzuri zaidi watazawadiwa pesa, medali, matengenezo ya maktaba ya shule pamoja na vitabu," aliahidi, na kuongeza kwamba maonyesho ya mwaka huu nayo yatadhaminiwa na Shell na pamoja na KJF.

Alisema udhamini wa Shell na KJF umewawezesha wanasayansi wa YST kutembelea shule na kuwafundisha wanafunzi namna ya kufanya utafiti na ugunduzi wa teknolojia.

"Tunawaomba walimu, wazazi, serikali, makampuni, asasi za kiraia kuendelea kuwasapoti wanafunzi hasa wakati huu ambao wanafanyia kazi ya utafiti wa kisanyansi na ugunduzi wa teknolojia," alisema.

# RC awataka walimu kufaulisha kwa 90%

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christine Mndeme, amewataka walimu wa shule za msingi na sekondari mkoani hapa kuona umuhimu wa kuongeza bidii katika kuwafundisha wanafunzi wao kwa lengo la kuongeza ufaulu kwa asilimia 90.

Katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Mkuu wa Wilaya ya Songea, Kamando Pololet Mgema, mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha tathmini ya elimu mkoani Ruvuma kilichofanyika wilayani Namtumbo ambacho kilihudhuriwa na walimu, viongozi mbalimbali wa serikali, pamoja na viongozi wa vyama siasa na wadau wa elimu, alisema tathmini ya utekelezaji wa kazi ni kipimo tosha katika kupima ufanisi wa shughuli yoyote.

Mndeme alisema katika kufanya tathmini ndipo unapoweza kubaini mafanikio na changamoto zilizopo na kuchukua hatua na kukabiliana nazo.

Aliongeza kuwa kufuatia kuwapo kwa tathmini hiyo, mkoa wa Ruvuma umejiwekea utaratibu wa kufanya tathmini ya maendeleo ya elimu kwa kuwashirikisha wadau wa elimu ngazi ya mkoa abapo kuanzia mwaka 2008 kumekuwapo pia na mikutano ya wadau ya tathmini ya maendeleo ya elimu ngazi ya wilaya, halmashauri, kata, na shule ambayo hufanyika kabla ya kikao cha tathmini ya elimu cha mkoa.

Aliwapongeza wakuu wa wilaya na wakurugenzi wote kwa kuonyesha ushirikiano kwa kufanya tathmini ya hali ya utoaji wa elimu katika maeneo yao.

# Taasisi yakagua mbegu 'feki'

**Na Futuna Seleman**

TAASISI ya kudhibiti ubora wa mbegu nchini (Tosci), imeendesha operesheni ya ukaguzi wa mbegu katika maduka ya wafanyabiashara jijini na kubaini baadhi kuuza mbegu zilizopitwa na wakati.

Aidha, imebaini baadhi ya maduka hayo kutumia kibali kimoja zaidi ya duka moja kinyume na utaratibu.

Ofisa Ukaguzi kutoka Tosci, Zera Mwankemwa, akizungumzia operesheni hiyo alisema inalenga kuhakikisha kuwa mkulima anapata mbegu bora iliyothibitishwa kwa ajili ya kilimo. Alisema katika operesheni hiyo baadhi ya mbegu zikiwamo za mahindi zimekutwa madukani zikiwa zimekwisha muda wake wa matumizi na hazina kibali cha kuonyesha kama zimeruhusiwa kuendelea kutumika baada ya kupimwa maabara na kuthibitishwa na Tosci zilichukuliwa katika zoezi hilo ili kuwanusuru wakulima ambao huzinunua na kuzilalamikia zinawatia hasara kwakuwa hazioti. "Katika ukaguzi huu tumeangalia mbegu zilizopo kama zimepitia katika udhibiti ubora na jinsi wafanyabiashara wanavyoendesha biashara hiyo kwa mujibu wa sheria na kanuni za mbegu nchini," alisema Zera na kuongeza:

"Vitu vinavyoangaliwa ni pamoja na kibali cha kuruhusu kuuza mbegu zinavyo hifadhiwa ili zisipoteze ubora wake, jinsi mfanyabiashara anavyotunza kumbukumbu za manunuzi na uuzaji wa mbegu kwa lengo la kumlinda mfanyabiashara na mkulima wapate mbegu kutoka kampuni halali zilizoandikishwa kuendesha biashara ya mbegu," alisema. Zera aliongeza kuwa wanachosisitiza kwa wafanyabiashara wa mbegu ni kuhakikisha kuwa wanafanya biashara hiyo kwa mujibu wa sheria na kanuni za mbegu nchini zinavyoelekeza.

"Wakulima wanaombwa kununua mbegu katika maduka ya mbegu yaliyosajiliwa, wasinunue mbegu ambazo hazina lebo maalum ya Tosci," alisema. Alisisitiza wakulima kuzingatia mbegu ambayo taarifa zote zikiwamo namba ya fungu ya mbegu ambayo inathibitishwa kuwa imepitia katika hatua zote za udhibiti asilimia ya utoaji wa mbegu, asilimia ya usafi pamoja na tarehe ya mbegu hiyo imefanyiwa majaribio ya mbegu ya maabara ili kupima ubora wake.

Aidha, alisema wafanyabiashara wa mbegu pamoja na wakulima iwapo wanaona tarehe hiyo ya majaribio ya mbegu imepita basi waombe kutoka kwenye kampuni zinazowasambazia kupatiwa kopi ya majaribio ya karibu ya kimaabara ili kujidhihirishia kuwa mbegu hiyo bado ipo kwenye ubora unaotakiwa.

"Vilevile wakulima wanunue mbegu ambazo hazijafunguliwa kwa kuwa mbegu za kupima zinaweza kuwa mbegu feki au zile ambazo zimeshapoteza ubora wake," alisema.

## HABARI ARUSHA

# Mwananke auawa akitaka kubakwa

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

REGINA Manday (35), aliyekuwa anafanya kazi kwenye shamba la mwekezaji Rift Wall Plantation Kijiji cha Magara Halmashauri ya Babati, ameuawa katika harakati za kubakwa.

Taarifa ya mama huyo kuuawa ilitolewa mwishoni mwa wiki na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Augustino Senga, na kusema tukio hilo lilitokea Aprili 15, mwaka huu saa 1:00 usiku, baada ya kupigwa mweleka na kuanguka chini. Kamanda Senga alimtaja mtuhumiwa wa mauaji hayo ni Claud Swedi maarufu kama Claud Safari (35), mkulima na Mkazi wa Kijiji cha Moya, na amekamatwa. "Chanzo cha mauaji haya marehemu alikuwa anakwenda kulala kambini kutokana na kufanyakazi za kibarua... wakati anapita maeneo ya korongoni kwenye mto, ndipo alipigwa mtama na kuangukia kisogo na kufariki dunia," alisema Senga.

Tukio hili limetokea mkoani hapa ikiwa ni wiki iliyowakutanisha wadau wa kupinga ukatili, ambao walikuwa wakijadiliana namna ya kudhibiti unaoendelea dhidi ya watoto na wanawake, hivyo kuwawekea mazingira rafiki ya kuishi na kufanya shughuli zao za kuwaingizia kipato bila woga.



Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Uingereza la Mpango wa Maendeleo nchini, Alice Motion (kushoto) akizungumza na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mshewe, Filbert Pelekamoyo, wakati wafadhili kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la kuwasaidia watoto alipotembelea shuleni hapo kusaidia miradi ya maji na usafi kupitia mradi wa SWASH. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Tanzania yashauriwa kutumia taasisi za kibenki kupaa uchumi

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

TANZANIA imebainika ndio nchi inayotumia huduma za kibenki kwa kiwango kidogo, ukilinganisha na baadhi ya nchi zingine za Afrika Mashariki na kushauriwa kuacha kuogopa kutumia taasisi za fedha, ili waweze kuinuka kiuchumi.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na afisa mwezeshaji kilimo fedha, kutoka Shirika la Taha, Angelina Nyansambo, ambaye alikuwa akiwajengea uwezo wakulima wa mbogamboga waliopo Halmashauri ya Babati ili waweze kubadilika na kuacha kuogopa kuzitumia taasisi za fedha.

Alisema utafiti uliofanywa hivi karibuni kuhusu watu wa nchi za Afrika Mashariki wanavyotumia huduma za kifedha, ulibaini kuwa Tanzania inatumia huduma za kifedha kwa asilimia 17, Rwanda asilimia 21, Uganda asilimia 28 na vinara ni Kenya ambayo wananchi wake wanatumia huduma za benki kwa asilimia 40.

Aidha, aliwataka wakulima hao kuchangamkia fursa ya kukopa katika taasisi za fedha, wakiwa tayari wameweka mipango mizuri ya kuwekeza katika kilimo biashara ili kilimo kiwe mkombozi wa maisha yao.

"Ila kama unakopa kwenda kufanya sherehe ndio mbaya au kama utakopa unataka kuongeza mke wa pili hiyo ndio itakuwa mbaya," alisema na kuongeza:

"Lakini ukikopa wakati unaenda kufanya mambo yako ya kilimo na ukafuata kanuni bora, kwa kupiga hesabu ya faida na hasara utafanikiwa."

"Kabla ya kukopa unatakiwa kufahamu riba yake siyo unakopa tu bila kujua marejesho, angalia kama unatengeneza faida kutoka kwenye mkopo siyo unakopa halafu unabaki pale pale, na mkulima unatakiwa uwe na tabia ya kujiwekea akiba, siyo ubaki kuwaza kukopa tu," aliongeza.

Aliwatajia madhara ya kutokuwa na elimu ya fedha kuwa ni kushindwa kupanua biashara, kutokufikia malengo, kutokufikia huduma za kifedha kwa urahisi, kutokufanya biashara kwa ufanisi na kuhama hama biashara bila mpangilio.

Said Siday, mkulima kutoka Kijiji cha Haraa alikiri kuwa Watanzania wengi hawana uelewa wa masuala fedha kwa sababu unakuta vikundi vingi vinatozwa riba ya asilimia tano, lakini benki zinatoza asilimia zaidi ya 15, lakini baadhi ya watu wanaacha vikundi wanaenda benki kwenye riba kubwa.

Aliishauri serikali kushusha riba akitolea mfano kwa benki ya NMB inatoza asilimia 15, hivyo aliiomba serikali ishushe kiwango hicho ili wananchi wasiogope kukopa na wajinufaishe na fursa zilizopo kwenye taasisi za kifedha na watoke kimaisha.

Mkulima mwingine, Rajab Mussa kutoka Kijiji cha Matufa, alisema Taha ni wadau muhimu na wamewatoa mbali kuhusu watu kuogopa kukopa, ila tatizo wanalokabiliana nalo ni ukosefu wa elimu ya kifedha," alisema na kuongeza:

"Ndio maana jirani wa Kenya wanawazidi katika kuzitumia taasisi za kifedha sababu wamefahamu kuchangamkia fursa."

Aliongeza kuwa wengi wao ni waoga, hivyo wanaona wanaweza kufilisiwa na taasisi za kifedha na kuogopa kukopa hasa pale wanaposhuhudia wenzao wanafilisiwa mali zao na na benki, tofauti na vikundi vinakuwa nafuu.

## Muro aingia mtaani kugawa vitambulisho

**Na woinde Shizza,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amefanya ziara ya kushtukiza kukagua zoezi la utoaji wa vitambulisho vya wajasiriamali na wafanyabiashara ndogondogo katika maeneo mbalimbali ya wilaya.

Baada ya kutoridhishwa na ugawaji, aliamua kuvigawa mwenyewe. Muro alilazimika kutoa elimu hiyo juzi kwa wafanyabiashara ndogo ndogo na wajasiriamali wa eneo la Soko la Tengeru, Usariver na Ngaramtoni, wakati wa ziara yake ya kushtukiza katika maeneo hayo.

Ziara hiyo ilizaa matunda kwa kuongeza mwitikio mzuri wa wafanyabiashara hao kuvichukua vitambulisho hivyo, baada ya kuelewa umuhimu wa kuvitumia.

"Kweli nimechukia kuona wafanyabiashara wengi hawana elimu juu ya vitambulisho hivi, licha ya Rais Magufuli kuvizungumzia kila mara, ila watendaji wangu hawatoi elimu ili watu waelewe, "alisema.

Alisema ni vema kila mmoja akahakikisha anakipata kitambulisho hicho ili kuepuka usumbufu katika biashara zake. Muro alisema ameamua kuvigawa baada ya kuona zoezi la utoaji vitambulisho hivyo limezorota, huku wafanyabiashara wengi wakiwa hawana uelewa umuhimu wa vitambulisho hivyo.

"Nimelazimika kuingia mitaani kutokana na kutoridhishwa na mwenendo wa utoaji wa vitambulisho hivi. Nimetoa maelekezo kwa wakurugenzi wa Halmashauri ya Meru na Arusha DC pamoja na maafisa tarafa na watendaji wa kata na vijiji kuacha tabia ya kuwasubiria wafanyabiashara maofisini na badala yake watoke na kuwafuata ili kuwapunguzia usumbufu wa kwenda umbali mrefu kuchukua vitambulisho hivi," alisema Muro.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa masoko ya Tengeru na USA River, Abia Mbise, alisema kuwa awali wafanyabiashara walikuwa na mwamko mdogo, kutokana na kutopatikana kwa urahisi kwa vitambulisho hivyo.

Alipongeza kitendo cha DC Muro kutoka ofisini na kuwafuata na kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuwa na vitambulisho hivyo, pamoja na kuvigawa mwenyewe, hatua iliyosaidia kuongeza mwitiko kwa wafanyabiashara wengi kuchukua vitambulisho hivyo.

# HABARI PICHANI



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Tanga Cement, Reinhardt Swart (katikati), na Meneja Rasilimali Watu wa kampuni hiyo, Diana Malambugi,wakikabidhi maboksi yenye vitu vya aina mbalimbali kwa baadhi ya watoto wenye mahitaji maalumu wanaosoma katika Shule ya Msingi Pongwe, katika hafla iliyofanyika shuleni hapo, Pongwe, Tanga hivi karibuni. Misaada hiyo ya vitu kama vyakula, nguo, sabuni na vitu vingine vilitolewa na wafanyakazi wa kampuni hiyo kama sehemu ya majukumu yao ya kuisaidia jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Wakazi wa jiji la Dar es Salaam wakipita karibu na meza iliyowekwa dagaa mchele ambao ni sehemu ya mboga maarufu kwa wakazi wake wa makundi mbalimbali. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Wafanyakazi wanaojenga barabara ya Magomeni kwenda Sinza Kijiweni wakiweka matuta kwa ajili ya kuzuia magari yaendayo kwa kasi hasa sehemu yenye watu wengi eneo la Kwa Mtogole jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Mkuu wa wilaya ya Arumeru Jerry Muro akiongea na Mganga mkuu wa halmashauri ya Meru, Petro Mboya mara baada ya kutoka kuwatembelea majeruhi waliopata ajali ya gari jana katika kijiji cha Oldonyosambu kilichopo wilayani Arumeru mkoani hapa ,ambapo jumla ya majeruhi wanne wamelazwa katika hospitali ya kanisa ya Selian. **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Wananchi wakijipatia mahitaji katika soko kuu la Majengo jijini Dodoma kama walivyokutwa walikuwa wakifanya maandalizi ya sikukuu ya Pasaka. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**



‘Hitaji’ mkataba wa EPA na kukua kwa viwanda



## Siri ya wanawake kufanikiwa katika viwanda barani Afrika



# Toleo maalum la Maendeleo ya Viwanda Tanzania

e
a

ia na
a gani
io ya-
chi na

kuzaji
oneka-
yesha
tenga
oja na
mpya

u kui-
limali
bazaji
no.

Mara,
eshaji
ukuaji
mitaji
nguvu
da vi-

a kiki-
kezaji
mae-
a Vik-
ua na
nzisha

kuwa
wakati
upitia
katika
John

gufuli
ifanya
amba
ufufua
vipya.
uwan-
Sep-
isema
vime-
agofu,
i kuvi-

sekta
kupe-
wake,
ilimia

gufuli
nda ni
itolea
limwa

amba
kubwa
kumu
aia na

*a ku-*
*andi-*
*simu*
*barua*



TEKNOLOJIA

NA CHARLES MASELE

SALEHBHAI GLASS INDUSTRIES LTD;

# Kampuni maridhawa biashara ya vioo na aluminiamu Tanzania

UNAPOONGELEA biashara ya vioo nchini Tanzania, moja kwa moja unakuwa unairejea Kampuni ya vioo ya Salehbhai, ambayo imejijengea jina kwa sasa linapokuja suala la biashara ya vioo.

Kampuni hii ni kati ya waanzilishi wa awali kwenye biashara ya vioo nchini. Ilianzishwa mwaka 1954, na ndani ya miaka 20 iliyopita imeweza kupanua huduma zake katika kila aina ya vioo na miradi mikubwa inayohusisha usimikaji wake.

Ina idara ya vioo, idara ya vioo vigumu vinavyozalishwa nchini vilivyo salama kwa maana ya kutoharibika kirahisi, ambavyo ni vya kwanza na vya aina yake vinavyotumia Teknolojia ya Ulaya.

Aidha, Kampuni pia ina aina ya vioo vya kivuli vinavyozalishwa nchini, na vioo vinavyozuia risasi kupenya, vyote vikiwa na kiwango na ubora wa Ulaya, vikitumia ubora wenye kiwango na usalama wa hali ya juu.

"Tunasambaza na kuweka ili kukidhi mahitaji kamili ya uhitaji wa vioo wa eneo lako la kazi, huku tukitumia wataalamu wetu wa ndani wenye maarifa na uwezo mbalimbali," anasema Mkurugenzi Mtendaji, Sajjad Salehbhai.

Salehbhai anasema kuwa miongoni mwa bidhaa zao ni:-

(a)Vioo vya nje vilivyofunikwa kwa nailoni maalumu kwa kuunganisha vizuri kati ya jengo na vioo kwa usalama na uimara ulio bora zaidi.

(b) Vioo vya mbele ya maduka na vinavyogawa vyumba vya maduka kwa vioo.

(c) Kugawa sehemu za ndani kwa vioo.

(d) Madirisha na milango ya kioo kimoja na vioo vilivyounganishwa pamoja kwa kutumia aina ya ubora wa hali ya juu wa vioo vya kudhibiti mwanga.

(e) Milango ya bafuni na vifaa vingine vya vioo vya bafuni.

(f) Vioo vya kuzuia ukuta kuharibika jikoni na bafuni.

(g) Milango imara ya vioo ya kusukuma kwa mashine, milango ya kusukuma na kukunja.

Mkurugenzi Salehbhai anataja baadhi ya kazi ambazo wameshazifanya na kusambaza hapa nchini kuwa ni;

- Vituo vya Mabasi ya Mwendo kasi Dar es Salaam (DART) amapo wameshasambaza zaidi ya mita za mraba 7,000 na vipimo maalumu vya ubora wa hali ya juu katika vipimo vya milimita nane aina ya bronze ya giza visivyoharibiwa kirahisi katika vituo vyote vya mabasi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Salehbhai Glass Industries Ltd, Sajjad Salehbhai. **PICHA: CHARLES MASELE**

> Kuajiri wafanyakazi wa hapa nchini ili kuendeleza ubora wa hali ya juu wa bidhaa za hapa.

- Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) kugawanya vyumba kwa vioo kwa ndani;
- Sehemu ya chumba cha maonyesho cha Kampuni ya Toyota Tanzania;
- Hotel ya Ramada Inn, Jangwani Blusters ambapo waliweka vioo vigumu;
- Ngazi za vioo imara (Grand stairs) milimita 38 visivyoharibika kirahisi vya rangi ya bluu vya ngazi vilivyotengenezwa hapa nchini kwa kuweka katika Hotel ya Ramada Inn, Jangwani.
- Kutenganisha vyumba kwa vioo katika ofisi za makao makuu ya UNICEF Tanzania.

"Kwa kutengeneza na kusambaza vioo vigumu na imara kwenye miradi hapo juu, tumeokoa gharama za kubadilisha fedha za nje kama waagizaji bidhaa hizo kutoka nje ya nchi wafanyavyo," anasema.

Salehbhai anasema muda wa kusubiri kwa vioo vigumu kutoka nje ya nchi ni takribani wastani wa wiki nane.

"Tunaweza kufupisha muda huo kuwa siku chache kwa kutengeneza hivi vioo hapa nchini, huku tukizingatia ubora wa hali ya juu katika kumaliza kazi ya mteja wetu kwa kuzingatia mahitaji yake kwa bei za ushindani... bidhaa zetu zimethibitishwa na Shirika la Viwango nchini (TBS)." anasema Salehbhai na kuongeza:

"Sisi pia ni wasambazaji tunaoongoza kwenye kila aina ya vioo vya ujenzi vyenye wembamba tofauti, rangi mbalimbali na aina mbalimbali za vioo."

Mkurugenzi huyu anabainisha kwamba kupitia kampuni yao kunapatikana pia vioo vya kujitazama, vya Luvasi, chuma za luvasi, vifaa mbalimbali vya milango na madirisha ya Aluminiamu na vifaa vya bafuni.

"Tukiwa na kiwanda chenye vifaa vya kisasa na mafundi waliobobea na kufunzwa, tunasambaza bidhaa zetu kwa kuzingatia matakwa ya wateja," anasema na kuongeza:

"Mafundi wetu wenye ujuzi wanatengeneza aina zote za Aluminiamu, na matakwa ya eneo kwenye sekta ya ujenzi."

Anabainisha kuwa wanafanya kila liwezekanalo kuhakikisha wanasambazia wateja wao bidhaa na huduma zenye ubora wa hali ya juu, kwa muda muafaka.

Aidha, Salehbhai anasema Kampuni yao imefanya kila linalowezekana na kuwekeza ili kuendana na kauli mbiu ya viwanda hapa nchini, badala ya kuendelea kutegemea kuagiza bidhaa kutoka nje na hivyo kuinyonya thamani ya fedha yetu.

"Kwa nini kuagiza kutoka nje na kuiweka fedha yako kwenye hatari, wakati tunaweza kukuzalisha kwa bei nzuri ya ushindani na kukupatia bidhaa zako katika kipindi kifupi." Anasema.

Anafafanua zaidi kwamba licha ya gharama kubwa za kutengeneza bidhaa, na changamoto za kimazingira hasa umeme, kampuni yao imewekeza na itaendelea kuwekeza kwenye teknolojia mpya.

"Lakini pia kuajiri wafanyakazi wa hapa nchini ili kuendeleza ubora wa hali ya juu wa bidhaa za hapa nyumbani zinazoonekana na endelevu na kuzingatia uthibiti wa upandaji wa gharama kutoka kwa wasambazaji wa nje ya nchi," anasema.

Mkurugenzi huyu anaungana na sera ya serikali kwamba maendeleo ya viwanda ndio njia pekee ya kuendeleza nchi ili kufanikisha malengo ya maendeleo.

Anasema Kampuni ya Salehbhai Glass itaendelea kufanikisha katika nafasi yake kwa kuwa mstari wa mbele kwenye sekta ya vioo na hatimaye kufanikisha malengo ya Taifa.

"Kwa nini uagize nje na kuweka fedha zako katika hatari wakati tunaweza kukutengenezea kwa bei nzuri za ushindani na kukuletea kwa muda mfupi,"anabainisha Salehbhai. TUNAKUBALI TENA!!

SALEHBHAI GLASS INDUSTRIES LTD

WAZALISHAJI WABOBEZI WA VIOO







Over 60 years in Glass Business never knowingly undersold on Price, specification, workmanship.

- Tunazalisha vioo vya kila aina.
- Vipo vioo kwa ajili ya kutengeneza fremu za maduka.
- Tunazalisha vioo vinavyofaa kazi zote za nje ikiwa ni pamoja na kweye ujenzi wa ghorofa, ofisi, hotel pamoja na nyumba za kawaida.
- Tunazalisha vioo vya rangi mbalimbali.
- Tunazalisha vioo visivyopenyeza risasi.
- Tunazalisha vioo vinavyoweza kutumika kwa namna yeyote ile.
- Tunazalisha vioo imara visivyovunjika hata kwa nyundo.
- Tunazalisha vioo vilivyobandana (double glass).
- Vioo vinavyotumika maliwatoni (shower doors and other bathroom).,
- Pia tunazarisha vioo vinavyotumika katika ujenzi wa jiko.
- Tunazalisha vioo toka mwaka 1954. Tunauzoefu wa kutosha kuliko kampunni yoyote inayojishughulisha na masuala ya vioo.
- Tumeenea nchi nzima, kupitia wawakilishi wetu. Tuna mashine za kisasa za kuzalisha vioo pia tuna wafanyakazi wazoefu na wenye ujuzi wa hali ya juu. Wasilisha mradi wako ili tukushauri na kukuhudumia kwa ustadi mkubwa na kwa haraka zaidi.

WASILIANA NASI

MTAA WA AGGREY/INDIRA GANDHI
S.L.P 40917
SIMU YA MKONONI: 0763 501 771
SIMU YA MEZANI +255 22 211 5859

FAX : +255 22 211 8896
EMAIL : salebhaiglass@hotmail.com
m.dawoodbhai@live.co.uk

XXXXXX

# Siri ya wanawake kufanikiwa katika viwanda barani Afrika

HAKI na usawa ndio mambo makuu yanayoshinikizwa duniani kila ulimwengu unapoidhimisha siku ya kimataifa ya wanawake.

Kwa kawaida siku hii huwa ni fursa ya kuchukua hatua, kufanya mabadiliko, kushinikiza, kuhimiza na kuwezesha wanawake wa nyanja zote kutambua uwezo wao.

Licha ya kwamba wanawake wanachangia ukuaji wa uchumi kote Afrika, ukandamizaji unakwamisha nafasi wanazoweza kuwa nazo.

Kutokana na kuendelea kukithiri kwa umaskini, wanawake wengi wanajikuta katika ajira zenye vipato vya chini na nafasi finyu ya kujiendeleza.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN), ili kuyafikia Malengo ya Maendeleo Endelevu kama sehemu ya ajenda ya mwaka 2030, kuna haja ya kulisaidia bara la Afrika katika kushinikiza ustawi endelevu wa viwanda na unaojumuisha kila mtu.

Hili linamaanisha kuwa hakuna atakayeachwa nyuma, hususan wanawake.

Baadhi ya mataifa ya Afrika yamepania kuwa nchi zilizoendelea kiviwanda, lakini mara nyingi idadi kubwa ya wanawake wanaonekana kususia kujitosa katika sekta hiyo.

Swali ni kwanini?

BBC ilizungumza na wanawake watatu kutoka Afrika Mashariki ambao ni miongoni wa wanawake wengi waliolivuka daraja hili na kupata ufanisi. Siri yao ni ipi?



Bertilda Niyibaho, mmiliki wa kiwanda kinachozalisha unga unaotokana na uyoga. **PICHA: MTANDAO.**

### BERTILDA NIYIBAHO KUTOKA RWANDA

Huyu ni mjasiriamali aliye na kiwanda kinachozalisha unga unaotokana na uyoga kufuatia mradi kabambe alioanzisha wa kuimarisha lishe bora miongoni mwa jamii.

Biashara yake imepanuka na kuvuka mipaka ya Rwanda.

Huku akionyesha kiwanda chake, ambayo sehemu kubwa ni maabara na sehemu nyingine inatumiwa katika kurutubisha zao la uyoga, anasema alianza kama mkulima tu wa kawaida:

"Nilianza shughuli zangu nikitengeneza pombe ya kienyeji itokanayo na ndizi, lakini nikaja kuona kwamba mabaki ya ndizi na mabaki ya mazao mengine yanatupwa tu kiholela ilhali yangeweza kuzalishwa mambo mengine yakawa na manufaa kwa jamii, basi nikajitosa katika kulima uyoga," anasema.

Kiwanda chake kilikua na akaanza kutengeneza unga wa uyoga na mazao mengine. Biashara yake imekua kadri muda unavyosonga mbele na imepanuka na kuvuka mipaka.

Kwa sasa yeye husafirisha bidhaa zake hadi Tanzania, Kenya, Uganda na hata Burundi. Licha ya ufanisi huu anasema hakukosa changamoto:

"Shida niliyonayo ni kwamba, bidhaa zangu zikifika huko mfano Uganda zinabandikwa leseni ya kwamba zilitengenezwa Uganda... binafsi nilifuatilia nikatembelea

> Pia inawawezesha wakulima kupata elimu ya kukuza biashara yao na kuona thamani ya kile wanachokifanya kwa kuboresha huduma zao na kutengeneza mnyororo mpya wa thamani.

wale wanaolangua bidhaa zangu nikashangaa nilipokuta kwamba wameandika eti 'Made in Uganda!" anasema.

Bertilda anataja changamoto nyingine kuwa ni kukosa kuungwa mkono na serikali na kupata leseni ya ubora wa bidhaa kumwezesha kupenya katika masoko ya Ulaya na Marekani.

### JENNIFER BASH KUTOKA TANZANIA

Huyu ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Alaska nchini Tanzania.

Kampuni yake imejikita katika kuongeza thamani kwenye mazao ya kilimo yanayozalishwa na wakulima wa Tanzania, wengi wao wakiwa ni wanawake.

Kampuni hii pia inajishughulisha na uzalishaji na usambazaji wa bidhaa za vyakula kama mayai, mchele, mafuta ya Alizeti, unga wa sembe na dona.

### SIRI YA UFANISI WAKE

Jenifer anaamini kwamba mtaji si kikwazo kwa kuwa wazo ndio mtaji.

"Mara nyingi watu wanakua na mawazo makubwa lakini wanashindwa kuyafanyia kazi wakidhani wanahitaji mtaji mkubwa kufanyia kazi mawazo yao,"anasema.

### UBUNIFU NI MUHIMU

Anasema kuwaza makubwa ni vyema, lakini ni muhimu kukubali kuanza na kidogo ili kufikia makubwa kulingana na mazingira yanayozunguka.

Jennifer anasema ubunifu wa uendeshaji wa biashara ni jambo muhimu kwenye kufanikisha biashara yeyote ili kupata wateja.

Mkurugenzi huyu anasema Alaska Tanzania imebuni soko lake kwa kujikita kwenye programu iitwayo 'Mama Alaska' ambayo inamuwezesha mama ntilie (Mama Lishe) kupata bidhaa za Alaska kwa urahisi na bei nafuu.

"Pia inawawezesha wakulima kupata elimu ya kukuza biashara yao na kuona thamani ya kile wanachokifanya kwa kuboresha huduma zao na kutengeneza mnyororo mpya wa thamani.

### LORNA RUTTO KUTOKA KENYA

Lorna Rutto ni mwanzilishi na Ofisa Mkuu Mtendaji wa EcoPost, kampuni ambayo imekuwa ikitumia taka za plastiki kuunda bidhaa mbalimbali zikiwemo boriti za kutumiwa kwenye mabango.

Kampuni yake huunda pia bidhaa mbalimbali za kutumiwa katika ujenzi. Lorna amepokea tuzo nyingi Kenya na kimataifa na alikuwa miongoni mwa wanawake vijana 20 wenye nguvu Afrika walioorodheshwa na jarida la Forbes.

Alipokuwa anaanzisha Ecopost, alikumbana na changamoto nyingi hasa katika kutafuta mtaji.

"Tulitazamwa kama biashara iliyo na hatari nyingi tukilinganishwa na biashara nyingine sokoni... Benki zilitaka taarifa za akaunti za benki kuthibitisha kwamba biashara yetu ilikuwa inafanya vyema ilhali tulikuwa tu ndio tunaanza," anasema na kuongeza:

"Tulitakiwa pia kutoa dhamana ya mkopo lakini hatukuwa na chochote."

Anasema waliwasilisha maombi katika mpango wa Enablis- uliofadhiliwa na Wakfu wa Safaricom na wakashinda na hapo wakafanikiwa kupata mtaji.

Mbali na fedha, Lorna anasema walikabiliwa pia na tatizo la mitambo ya kutumia ambayo walihitajika kuiagiza kutoka nje ya nchi, pamoja na wafanyakazi wenye ufundi uliohitajika kuendesha mitambo hiyo.

Anabainisha kwamba gharama ya uzalishaji ilikuwa pia juu, yaani gharama ya umeme, malighafi, kulipia leseni na zinginezo.

"Hatukupokea pia usaidizi kutoka kwa serikali na wanaounda sera... Wajasiriamali hasa walio katika sekta ya viwanda wanahitaji kichocheo na usaidizi pamoja na mazingira mahsusi ili kufanikiwa," anasema na kuongeza:

"Niliigundua fursa yangu katika kutumia tena taka... Taka si taka hadi zitupwe, kazi yote pia ni ya heshima... Nimejifunza pia kwamba ni muhimu kuwa mbunifu, kuvumbua na kuendelea kujiboresha kila wakati."

Anafafanua kuwa safari yake haijakuwa rahisi lakini amejifunza kutokata tamaa na kuwa amegundua kwamba kuomba msaada inapobidi ni muhimu.

Lorna anasema wanawake wengi hufikiria kwamba kuomba msaada ni dalili ya udhaifu.

"Ukweli ni kwamba ni ishara ya nguvu... Kupata washirika wafaao ni muhimu pia... Ukitaka kwenda haraka, nenda peke yako, ukitaka kwenda mbali, shirikiana na wengine," anasema.

Ushauri wake kwa wanawake ambao wangependa kufanikiwa katika viwanda ni kwamba, lazima kutafuta soko la bidhaa kwanza.

"Ningewahimiza wanawake wawe wabunifu na kuvumbua mambo na pia kuingia katika sekta ambazo zimetawaliwa na wanaume kwa muda mrefu mfano viwanda wakiona kuna fursa," anasema na kuongeza:

"Usiige tu wengine au kuchagua biashara iliyo rahisi... Soko limejaa wahusika wengi na kuna changamoto katika kutafuta nafasi ya ukuaji."

Anashauri wanawake wawe na ujasiri na waanze mara moja bila kukawia.

"Usizuiwe na chochote, usizuiwe hata na mtaji... Ningewashauri wanawake kuanza na fedha walizonazo na kuzitumia vyema," anasema.

Anabainisha katika kuanzisha biashara au kiwanda, ni vyema kufikiria mchango wa biashara hiyo kwa jamii.

"Moja ya yaliyosaidia ukuaji wa Ecopost ni nia yetu ya kutaka kuleta mabadiliko katika jamii, tukihifadhi mazingira pia," anasema. **BBC**

VIWANDA

NA NIMI MWETA

# ‘Hitaji’ mkataba wa EPA na kukua kwa viwanda

UWEZEKANO wa kutiwa saini mkataba wa ushirikiano wa karibu kiuchumi kati ya Umoja wa Ulaya (EU) na nchi za makundi tofauti ya ushirikiano kiuchumi Afrika unaendelea kuimarika.

Hiyo ni baada ya Tanzania kuthibitisha kuwa iko katika majadiliano ya mwisho na EU ili kutia saini kuanza kutumika kwa mkataba huo.

Tayari Rwanda na Kenya zilishatia saini kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wakati Uganda na Tanzania zimekuwa zikiwasiliana kuwa na msimamo wa pamoja, lakini baada ya Kenya na Rwanda kutia saini, ni suala la kuendeleza Jumuiya iliyopo au iparaganyike. Ndicho inaelekea kiliamuliwa, kuwa waliobaki wasaini mkataba pia.

Suala la kuwapo makubaliano ya mfumo mpya wa uhusiano wa kiuchumi kati ya nchi za Afrika na Ulaya lilianza rasmi mwaka 2000.

Ni wakati jopo la kusikiliza rufani na madai ya kibiashara kati ya nchi tofauti la Shirika la Biashara la Umoja wa Mataifa (WTO) lilipokubali ombi la Marekani kuwa mahusiano ya kiuchumi kati ya EU na makoloni yake ya zamani barani Afrika yarekebishwe, ili nchi hizo zisipewe nafasi maalum katika biashara na Ulaya, tofauti na nchi maskini nyingine duniani.

Ikabidi Umoja wa Ulaya uweke kiwango cha kipato kama msingi wa kuingiza vitu bila kodi na bila mkataba wa kupeana nafasi za aina hiyo.

Mzozo huo ulikuwa vile vile ishara kuwa biashara kati ya nchi za Ulaya na Afrika inaondoka katika hali ya kutoa nafasi ya kuuza vitu bila ushuru kama ridhaa ya kusaidia maendeleo yake, kuwa suala la kimkakati.

Nchi za Amerika ya Kusini ambazo zina ushirikiano wa karibu na Marekani zilitetewa na Mare-

INAENDELEA UK.20



Moja ya viwanda vya maua mkoani Arusha, vilivyo na nafasi ya kufaidikka zaidi endapo mkataba wa EPA utafikiwa. **PICHA: MTANDAO.**


## MEAT KING

## BIDHAA BORA ZA NYAMA ZA KITANZANIA “HapaNyamaTu”

King Bongo HAPA NYAMA TU Sausage



Meat King imekuwa ikizalisha bidhaa mbalimbali za Nyama katika kiwango cha juu cha Ubora kwa ajili ya Sekta ya Ukarimu ya Kitanzania ( Hospitality Industry) tangu mwaka 1995 na imekuwa ikitunukiwa tuzo ya juu ya Kampuni 100 za saizi ya kati nchini kila mwaka, tangu mwaka 2014.

Kutokana na uhitaji wa soko la Kitanzania la kuzalisha bidhaa zenye ubora na virutubisho lishe kwa kutumia Nyama ya Tanzania ili kuwa mbadala wa bidhaa ghali za nyama zinazoagizwa kutoka nje, sambamba na uhamasishaji wa Serikali wa ‘Tanzania ya viwanda’ hasa kwenye sekta ya ufugaji ambayo imekuwa na ongezeko dogo sana la thamani, Meat King imetanua uendeshaji wake wa biashara kwa kujenga kiwanda kikubwa cha kuzalisha na kusindika nyama chenye ukubwa wa eneo 1216m2 mkoani Arusha (Moshono).

Kiwanda kilianza kazi zake mnamo Juni 2017 na kilifunguliwa rasmi na kuanza kazi mnamo tarehe 5 mwezi wa Septemba mwaka huo huo, wakati wa sherehe za kuwasha Mwenge wa Uhuru Kitaifa. Meat King haina machinjio, hivyo wanyama wote wanachinjwa katika machinjio yaliosajiliwa na kusimamiwa na maafisa wa mifugo ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa bidhaa zenye afya na ubora.



MKD inazalisha zaidi ya bidhaa 100 za nyama zilizo safi/fresh na zilizosindikwa zitokanazo na nyama ya ng’ombe, kondoo, kuku na nguruwe ambazo ikiwa ni pamoja na nyama za aina zote zilizo tayari kwa kuliwa , soseji, nyama zilizokaushwa/bekoni, nyama zilizotibiwa/cured meats salami, procuitto, nyama zilizostawishwa- ambayo ni TTT (Tanzanian Taste without the Toughness), aina za nyama za steki (nyama bila mfupa), delicatessen na aina za nyama za kibongo zilizoongezwa thamani zilizojikita kwenye kuhudumia Sekta ya Ukarimu (Hoteli, Lodges, matukio na sherehe mbalimbali) kwa Watanzania.

Meat King ina Maeneo mawili ya Uzalishaji, ambapo kila eneo lina mapokezi yake pamoja na sehemu yake ya kusindika na kuhifadhi bidhaa za nyama. Kuna upande wa Nyama ya ng’ombe, kuku na kondoo ambao ni halali na upande wa nguruwe na bidhaa zisizo halali ili kuwezesha uzalishaji na uhifadhi kufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Halal.

Kiwanda kina uwezo mkubwa wa kuzalisha hadi Kilogramu 920,000 kwa awamu moja. Mipango ya Uwekezaji inafanyika ili kujenga eneo tengefu la uzalishaji na usindikaji wa bidhaa Halal ambapo uwezo wa Uzalishaji na usindikaji utakuwa na kufikia Kilogramu 2,500,000 kwa mwaka na kutufanya Meat King Distributors kuwa wazalishaji wakubwa zaidi wa Bidhaa Bora za Nyama Tanzania.

Kiwanda ni rafiki kwa kutunza mazingira, kina Bwawa kubwa kwa ajili ya ukusanyaji maji ya mvua, matumizi ya nishati ya jua kuchemshia maji, mfumo wa gylcol wa viyoyozi, na misitu wa magugumaji kwa ajili ya kuzalisha upya maji ya taka (sewage recycling) kwa ajili ya kutumia kwenye umwagiliaji wa bustani kupendezesha mandhari ya Kiwanda.

Meat King inafanya kazi kwa ukaribu na zaidi ya wakulima na wasambazaji 800 wa nyama nchini ili kuboresha uzalishaji/uzaaji, ulishaji na jinsi ya kuwatunza wanyama kwa kiwango kinachotakiwa katika uzalishaji wetu. Tunawakagua wakulima na kuhakikisha kuwa wanyama wanatunzwa kwa hali ya kiubinadamu, kuku wanakuwa na uwezo wa kuwa huru(kukimbia kwa kujitafutia chakula wenyewe) na sio kulishwa vyakula vya samaki ambapo huharibu ladha ya nyama ya kuku, hawapewi madawa ya kuwakuza haraka (hormones) na matumizi ya madawa mengi.





*sehemu za vituo vya machinjio zilizowekwa alama za rangi ili kuzuia muingiliano wa bidhaa.*

Kampuni inafanya kazi bega kwa bega na mamlaka za ndani na wadau katika sekta ya usindikaji wa yama na imekuwa ikipokea usaidizi mzuri sana kutoka kwa serikali na mamlaka za chini ili kukuza sekta ya nyama.

Kampuni inamilikiwa na kusimamiwa na mwanamke kwa kiasi kikubwa, na kikosi madhubuti cha wafanyakazi zaidi ya 60 hivyo kuleta ujuzi na uzoefu wa ndani na nje ya nchi katika sekta ya usindikaji nyama.

**Meat King Distributors Ltd**
**S.L P.13343,**
**Barabara ya 881 Nelson Mandela - Moshono**
**Arusha, Tanzania**
**orders@meatking.co.tz**
**+255 788 686 558 , +255 746 003 300**
**www.meatkingtz.com**

215187102

VIWANDA

# ‘Hitaji’ mkataba wa EPA na kukua kwa viwanda



Viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Kutoka Kushoto ni Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya, Yoweri Museveni wa Uganda, John Magufuli wa Tanzania na Paul Kagame wa Rwanda. **PICHA: MTANDAO**

**INATOKA UK.19**

kani katika WTO na baada ya hapo Marekani ikatoa nafasi kama ya EU kwa nchi za ‘Afrika, iitwayo AGOA.

Imedumu kwa miaka zaidi ya 15 na kila wakati inajadiliwa na Bunge la Marekani kama iendelezwe kwa kipindi kingine cha miaka minne au nchi za Afrika ziingizwe katika kanuni za kawaida za biashara. Bado mpango huo unaendelea.

Kuelewa kuwa siyo jambo rahisi kuoanisha zinachotaka nchi za Ulaya na matazamio ya Afrika katika suala hilo, inatosha kuangalia urefu wa majadiliano hayo, ambako watafiti wa masuala ya biashara wanasema yalianza kikamilifu mwaka 2002.

Lengo lilikuwa kufikiwa mkataba wa EPA (ushirikiano wa karibu kiuchumi, aina ya ubia) kati ya Ulaya na Afrika mwaka 2007, miaka saba baada ya uamuzi wa jopo la WTO kubatilisha mfumo uliokuwepo awali.

Kuanzia wakati huo maangalizo tofauti na ‘tarehe za mwisho’ zimewekwa na kupita, na licha ya kutiwa saini mkataba huo hapa na pale, bado haujawa sehemu mahsusi ya biashara Afrika hadi hivi sasa.

Wakati ambapo hivi sasa kuna hali ya kukubalika kwa mkataba huo (au mikataba hiyo kwani ni maeneo tofauti yenye mifumo ya kikanda ya ushirikiano kiuchumi inayoingia mkataba), kilichobadilika hasa ni mwelekeo wa taswira ya uchumi barani Afrika.

> “Kusema itazuia maendeleo si sahihi, bei ikiwa ndogo watu wananunua vitu zaidi tena vya kila aina, ambayo inakuwa ni kichocheo cha kujenga na kuendeleza viwanda.

Tatizo katika miaka yote hii ilikuwa ni kuoanisha hitaji la ujenzi wa viwanda barani Afrika na kuingia mkataba na Ulaya ambako bidhaa zao zitatosheleza soko la Afrika.

Hatua ambayo wengi kati ya wataalamu na hasa vikundi vya wanaharakati barani humu viliwatia hofu wanasiasa na wananchi kwa jumla kuwa itazuia kukua kwa viwanda katika nchi hizi. Ni mjadala mrefu lakini wanaharakati walishinda.

Hivi karibuni, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Pofesa Palamagamba Kabudi aliwaambia wabunge kuwa serikali iko katika hatua za mwisho za kujadiliana na Umoja wa Ulaya kuhusu vipengere nyeti kadha wa kadha kwa nia ya kutia saini mkataba huo majadiliano hayo yakikamilika.

Suala kwa wanaharakati siyo tu kwa hapa nchini lakini pia katika Umoja wa Ulaya, si vipengere husika ila suala zima la kuingia mkataba huo. Hiyo ni kwa sababu taswira ya uchumi wa nchi unaokua kwa ndani na kutumia tu soko la nje kuuza bidhaa na kuvutia mitaji kujenga viwanda nchini, bado inatawala katika hisia za wanaharakati.

Wale wa hapa nchini wakamwita mwenzao, Profesa Helmut Asche wa Ujerumani kupigilia msumari ‘tusisaini.’

Tatizo la majadiliano hayo na hata hitaji la kumwita mtaalamu huyo Profesa wa siku nyingi Chuo Kikuu cha Leipzig na mzoefu wa masuala ya uchumi barani Afrika, ni kutaka hatima ya kuanza kutumika mkataba huo ijulikane wazi, na ithibitishwe katika mkataba.

Ni kutaka aina fulani ya matokeo iwekwe bayana, wakati ambapo mkataba wa ushirikiano ni kuweka mifumo ya kurahisisha biashara, uwekezaji, ununuzi wa rasilimali, kuingiza na kutoa fedha, kuingia na kutoka kwa wataalamu, urahisi wa kupata kibali cha kuishi na baadaye uraia kwa watakaotaka, n.k.

Siyo kuhakikisha kuwa viwanda vyetu vitamudu ushindani na bidhaa za nje, vyote au baadhi.

Suala la kujua ni viwanda gani vitamudu ushindani na vingapi vitakufa na baada ya hapo itakuwaje haliwezi kumalizwa katika meza ya majadiliano kwani kimsingi ni suala la soko, linalotegemea ufanisi wa mjasiriamali au mwekezaji husika, uadilifu wa utawala katika uendeshaji wake, n.k.

Ndiyo maana kilichoamua suala hilo liende vipi ni kitu tofauti kabisa, kuwa wapo waliokubali kutia saini wakijua kuwa mkataba una faida nyingi na fursa lukuki, kwa mfano wananchi wa Afrika Mashariki kupata bidhaa za Ulaya kwa bei poa, si makodi yajazwe pindi zinapofika bandarini.

Kusema itazuia maendeleo si sahihi, bei ikiwa ndogo, watu wananunua vitu zaidi tena vya kila aina, ambayo inakuwa ni kichocheo cha kujenga na kuendeleza viwanda.

Halafu tusiposaini, tutafunikwa na magendo, bidhaa nzuri za bei poa zikifurika nchini kupitia ‘njia za panya,’ bila faida ya mkataba, misaada husika.

Kuna upande mwingine wa suala hilo ambao inawezekana ukaanza kujulikana au kuangaliwa kwa jicho la karibu zaidi baada ya mkataba wa EPA kutiwa saini kuwa Mwalimu Nyerere aliota na kupigia debe hali kama hiyo, lakini kwa kukazia hofu kuwa haitawezekana.

Aliona jinsi nchi za Ulaya Mashariki zilivyoinuka kwa haraka kiuchumi baada ya kuanguka kwa ukuta wa Berlin mwaka 1989, au nchi za Mashariki ya Mbali zilivyokua kwa haraka miaka ya 1980 kutokana na uhusiano wa karibu wa kupokea mitaji kutoka Marekani, wakiingia ubia na wenyeji, kama China iliyopiga hatua baadaye,

Malaysia, Dubai, n.k. Wanaharakati wanakazia kuimarisha mfumo wa elimu ili kufikia viwanda, wakati kuingia ubia na kununua kampuni za hapa nchini bila vizuizi ndiyo njia inayofahamika kuleta tija ya haraka ya kukuza viwanda.

Tuangalie tusije tukafunikwa na magendo viwanda, tuwe kama Haiti ilivyo katika eneo la Caribbean, kisiwa cha umaskini katika eneo la utajiri.



## Mchungaji awaonya waumini wanao hamahama makanisa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAUMINI wa dini ya Kikristo nchini, wameshauriwa kuacha tabia ya kuhamahama makanisa kwa madai ya kutafuta uso wa Mungu na nguvu za uponyaji badala yake waishi maisha ya imani na msimamo.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mchungaji wa Kanisa la Hema ya Maombi, linaloongozwa na Mtume, John Gondwe, lilipo katika Kata ya Iyela, jijini Mbeya kwenye ibada ya Pasaka.

Mtume Fredy alisema kuhamahama makanisa sio suluhu ya kupata uponyaji wala kuwa karibu na uso wa Mungu bali matendo ya mtu na imani yake ndio itamponya. "Nyakati hizi ni tofauti na zamani, sasa hivi waumini wanatangatanga na makanisa, leo kanisa hili, kesho lile, ukimuuliza anakuambia kule hakuna Mungu ni dhambi kubwa, Mungu yupo kila mahali hata hapo ulipoanza kuabudia yupo usiondoke," alisema Mtume Fredy.

Alisema katika kusherehekea sikukuu ya Pasaka, Wakristo wanapaswa kuzitafakari njia zao na kuacha maovu ikiwamo mauaji, wizi na visasi kwa kuwa Yesu alitoa uhai wake kwa ajili ya kumkomboa mwanadamu.

Aliongeza kuwa baadhi ya waumini sio wavumilivu wanapokutana na misukosuko, huhama makanisa au kuacha ibada na huko hukutana na ibilisi anayezidi kuwatesa. "Nawashauri kusimama katika maombi na kuendelea kumshukuru Mungu."

Alisema kila jambo lina majira yake hivyo Mungu ana uwezo wa kubadilisha jambo lolote lililoonekana gumu hata kama ni magonjwa, kuyumba kiuchumi na hata maadui wanaokufuatilia badala ya kwenda kwa waganga.

Aidha, aliwasisitiza watoto wa kike kusimamia misingi ya Kitanzania ambayo inadumisha mila na desturi zinazokubalika kuanzia kwenye mavazi na tabia na kuacha kuiga mitindo ya mataifa mengine.

Alisema mabinti wa nyakati za sasa hawana maadili, wanavaa mavazi ya aibu ambayo yanawapa vishawishi wanaume kuwabaka, aliwaomba kuvaa mavazi ya staha.

# Asiyetoa risiti kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imesema itamchukulia hatua za kisheria ikiwamo kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi mfanyabiashara yeyote ambaye atabainika hatoi risiti za manunuzi kwa mteja.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Kamishna wa Kodi za Ndani, Abdul Zuberi, katika kikao cha watumishi wa TRA na wafanyabiashara kilichofanyika mwishoni mwa wiki jijini Mbeya.

Zuberi alisema baadhi ya wafanyabiashara sio waaminifu kwenye biashara zao na badala yake huiibia serikali kwa kutotoa risiti za manunuzi wa wateja wao.

Alisema kitendo hicho sio cha kizalendo bali kinalengo la kuibia serikali mapato na kwamba atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alitoa rai kwa wafanyabiashara kote nchini kufanya biashara zao kwa kufuata kanuni na taratibu na kuwa waaminifu katika ulipaji wa kodi ili fedha zinazokusanywa zitumike kwenye shughuli za maendeleo.

"Kama kuna mfanyabiashara yeyote ambaye anauza bidhaa zake bila kutoa risiti aache mara moja ukikamatwa utakuwa na kesi ya kujibu kuhusu uhujumu uchumi, nawashauri zingatie kanuni na sheria zilizowekwa kwenye kodi ili mfanye biashara zenu kwa uhuru," alisema Zuberi.

Katika hatua nyingine Zuberi aliwashauri wafanyabiashara kutokuwa wepesi wa kulipa kodi kwa watu wanaodai wanakusanya kodi kwenye maeneo ya biashara zao na badala yake wawe makini na ikiwezekana kufika katika ofisi za TRA kulipa.

Alisema baadhi ya watumishi wa serikali sio waaminifu, hutumia mwamvuli wa TRA kuwaibia wafanyabiashara, hivyo aliwataka kuwa makini kulipa kodi.

"Mfanyabiashara kama unamashaka na mtumishi anayekusanya kodi usimpe badala yake fika kwenye ofisi za mamlaka ndipo utoe na uhakikishe unapewa risiti," alisisitiza Zuberi.

Baadhi ya wafanyabiashara akiwamo, Peter Mwalongo, aliiomba TRA kuangalia upya gharama za kodi ya majengo ambayo inadaiwa kuwaumiza baadhi ya wananchi.



Meneja wa Biashara na Mkakati wa Mauzo wa Vodacom Tanzania Plc, kanda ya Dar es Salaam na Pwani, Caleb Majo (kushoto), akizungumza na wanafunzi wa Chuo cha Uongozi wa Fedha (IFM), wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo na uelewa wa teknolojia za kifedha jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Semina hiyo imefanyika chini ya Vodacom Tanzania Foundation kwa kushirikiana na Taasisi ya Green Hope ili kuhakikisha wanafunzi hao wanapata ufahamu wa teknolojia hizo na mchango wake katika kuchochea ushirikishwaji wa kifedha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Unywaji pombe mjamzito ni ukatili wa mtoto tumboni

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, amewaonya wajawazito kuacha matumizi ya pombe ambayo yanatajwa kama aina ya ukatili kwa mtoto aliyeko tumboni.

Akizungumza na Nipashe, aliwataka wajawazito wanaokunywa pombe kutambua kuwa wanawafanyia ukatili watoto walioko tumboni ambao kimsingi hawana hatia.

Kisemba alisema aina hiyo ya ukatili kwa mtoto aliyeko tumboni huchangiwa na mambo mbalimbali ikiwamo ukosefu wa elimu kuhusu athari za unywaji pombe, wajawazito kuamini unywaji wa pombe huimarisha afya ya mtoto tumboni.


"Unywaji wa pombe kwa mama mjamzito ni kosa na miongoni mwa aina za ukatili, dhidi ya mtoto aliyeko tumboni ambaye kupitia pombe hizo anaweza kupata udumavu ambao utamsababishia madhara ya kimwili na kifikra," alisema Kisemba.

Alisema mtoto atakapozaliwa anaweza kukosa uwezo wa kufikiri vizuri na kumfanya kuwa zezeta kutokuwa mchangamfu na ukuaji wake unakuwa wa kusuasua.

Aliwaomba ajawazito kuacha matumizi ya pombe, pia wadau vikiwamo vituo vya taarifa na maarifa kuendelea kutoa elimu ya athari hizo na kufuata ushauri wa kitaalam.

Alishauri vituo vya taarifa na maarifa kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwamo TGNP-Mtandao kuelimisha jamii aina za ukatili wa kijinsia, malezi na makuzi kwa mtoto.

Mwenyekiti wa vituo vya taarifa na maarifa wilayani Mbeya, Flora Mlowezi, alisema wajawazito wengi wanaokunywa pombe ni mabinti ambao kimsingi hawana elimu ya kutosha kuhusu afya ya uzazi.





# Askofu awataka Watanzania kutunza chakula

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Kimethodost Tanzania, Joseph Bundala, amewataka Watanzania kutunza chakula ili kujiepusha na baa la njaa kutokana na mvua kunyesha chini ya kiwango katika msimu huu wa kilimo.

Bundala aliyasema hayo juzi wakati akihubiri kwenye ibada ya Sikukuu ya Pasaka iliyofanyika katika Kanisa Kuu Ipagala, jijini Dodoma.

Aliwataka Watanzania kujiepusha pia na matumizi yasiyo ya lazima yanayotumia nafaka kama upikaji wa pombe, ngoma za unyago na mikusanyiko ya misiba.

Alisema kuwa kwa mwaka huu mazao katika maeneo mengi yamekosa mvua za kutosha, hivyo waliobahatika ni vizuri wakahifadhi chakula hicho kwa ajili ya matumizi ya msimu ujao.

"Pamoja na serikali kuwa na akiba ya kutosha ya chakula, lakini ni vizuri pia kwa Watanzania wakaepukana na matumizi yasiyo ya lazima ambayo yanaonekana kuwa ya anasa ikiwamo upigaji wa pombe za kienyeji," alisema Bundala.

Pia kuwaomba Watanzania kuombea uchanguzi wa serikali ya mtaa utakaofanyika mwaka huu mwishoni, ili waweze kupatikana viongozi watakaotokana na baraka za Mungu.

Alisema kumekuwapo na tabia za vitendo vya kishirikina pindi inapofikia chaguzi mbalimbali kwenye vyama vya siasa kwa wagombea kwenda kwa waganga wa kienyeji badala ya kukimbilia katika nyumba za ibada ili waombewe.

Alisema kuwa kutokana na tabia hiyo ni muhimu kwa waumini ndani ya nyumba za ibada wakaomba kwa ajili ya uchaguzi huo ili viongozi watakaojitokeza waache kwenda kwa waganga hao wa kienyeji, mara nyingi wamekuwa wakisababisha kupatika viongozi wasio kuwa na maadili ya kiroho.

Aidha, amewashauri viongozi wa dini kuendelea kukemea vitendo viovu vitakavyojitokeza kwenye chaguzi hizo, hata kama miongoni mwao wanatoka kwenye makanisa yao.



Baadhi ya Wakazi wa Jjiji la Dodoma, wakifanya manunuzi ya kuku katika shamrashamra ya Jumatatu ya Pasaka soko kuu la Majengo jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Machinga watakiwa kufuata taratibu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA ndogondogo maarufu (wamachinga) jijini Dodoma, wanaofanya shughuli zao katika maeneo yasiyo rasmi wametakiwa kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa na halmashauri ya jiji hilo kwa kuondoka katika maeneo hayo haraka.

Agizo hilo la jiji limetokana na operesheni maalum ya kuwapanga wafanyabiashara katika maeneo rasmi ikiwamo katika masoko husika.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alisema kuwa kwa mujibu wa mipango ya halmashauri yapo maeneo rasmi yaliyopangwa kwa ajili ya biashara na siyo barabarani wala yale yasiyo rasmi.

"Kwa jitihada kubwa zinazofanywa na halmashauri ya jiji, hivi sasa yapo maeneo mengi rafiki kwa shughuli za kufanya biashara ikiwepo kwenye masoko kama vile Bonanza, soko kuu la Majengo, Sabasaba, Chang'ombe na soko maalum la jioni Nyerere square," alisema.

Yuna aliongeza kuwa ni vema masoko hayo yakatumika kwa wafanyabiashara hao badala ya kuzagaa mitaani na barabarani ambako wanaweza kusababisha majanga ya ajali kwa watembea kwa miguu kukosa uhuru suala ambalo linaweza kuchangia hasara kwao.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara hao kuzingatia maelekezo sahihi ya halmashauri ya jiji ili biashara zao ziwe na tija kiuchumi.

Hata hivyo, ofisa masoko huyo alisema kuwa uwepo wa wafanyabiashara kwenye maeneo hayo yasiyo rasmi kunachangia kuzangaa kwa taka hovyo kwa kuwa utaratibu huo hautokani na mpango wa halmashauri ya jiji.

## Kituo cha polisi chapata askari baada ya miaka 25

**Na Paul Mabeja,** BAHI

KITUO cha polisi kilichojengwa kwa nguvu za wananchi katika Kijiji cha Chipanga A, Kata ya Chipanga, Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma miaka 25 iliyopita, kinatarajiwa kufunguliwa hivi karibuni baada ya kupangiwa askari.

Hayo yalibainishwa na Mbunge wa Jimbo la Bahi, Omar Badweli, wakati wa ziara ya kamati ya utekelezaji ya umoja wa vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM), Mkoa wa Dodoma walipotembelea kata hiyo kuangalia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya mwaka 2015.

Badweli, alisema kituo hicho kilijengwa miaka 25 iliyopita wakati akiwa diwani wa kata hiyo, lakini hakijawahi kufunguliwa licha ya kuleta mawaziri na makamanda polisi.

"Habari nzuri ni kwamba sasa wakazi wa eneo hili nimepokea simu kutoka makao makuu ya jeshi la polisi kuwa kituo hichi kimepangiwa askari na kitafunguliwa wakati wowote kuanzia sasa," alisema Badweli.

Aidha, alisema ameshaitisha mkutano wa tarafa nzima ili kupeana taarifa kuwa wanatakiwa wakutane pamoja ili kukifanyia ukarabati kituo hicho kianze kufanya kazi.


Naye, Mbunge wa Viti Maalum anayewakilisha vijana, Mariam Ditopile, alisema atatumia ushawishi wake kuhakikisha kuwa miradi mikubwa inafika katika kata hiyo.

Aliongeza kuwa pia atahakikisha kuwa tatizo la umeme katika miradi ya maji linalolalamikiwa na wanachi hao linakwisha ili wananchi waweze kupata huduma ya majisafi.

"Niwahakikishie umeme utafika hadi kwenye mradi wa maji, hiyo ndio sababu ya REA awamu tatu itagusa vijiji vyote na kuingia kwenye miradi ya maendeleo, kwahiyo lazima umeme ufike kwenye mradi," alisema Ditopile.

Katika kijiji hicho Mbunge Mariam Ditopile, pia alitoa mifuko 10 ya saruji kwa ajili ya zahanati ya kijiji, Sh. 150,000 ya kuchangia upauaji wa darasa la shule ya msingi na Sh. 150,000 kwaajili ya kuchangia ujenzi wa nyumba ya walimu.

HABARI ZANZIBAR





Mwendesha bodaboda akisafisha pikipiki yake katikati ya barabara iendayo Kariakoo eneo la Jangwani ambalo limejifunga kutokana na mvua inayoendelea kunyesha jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Balozi Seif aeleza matumaini mradi ujenzi majengo ya shule

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alisema mradi wa ujenzi wa majengo mapya ya Shule za Sekondari za Ghorofa unaofanywa na Serikali katika maeneo tofauti Zanzibar utakapokamilika utasaidia kuondosha changamoyo za uhaba wa madarasa.

Alisema mradi huo uliopangwa kutekelezwa katika shule zipatazo 20 kila wilaya pamoja na yale maeneo yenye idadi kubwa ya wanafunzi wa sekondari italeta faraja kubwa kwa wanafunzi na wazazi.

Balozi Iddi alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na uongozi wa kamati za shule za sekondari za Mahonda na Fujoni pamoja na walimu alipofanya ziara ya kukagua kumbi mbili za kufanyia mitihani za shule hizo zilizojengwa kwa nguvu za wananchi na walimu.

Alisema Serikali kupitia Sera ya Elimu imejizatiti katika kuongeza majengo ya shule kwa lengo la kukidhi mahitaji halisi ya ongezeko kubwa la idadi ya watu nchini.

Balozi Iddi alisema wakati Serikali ikiendelea na harakati zake za kujenga miundombinu katika sekta ya elimu, uongozi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (Tasaf ) unaoratibiwa na Ofisi yake kwa upande wa Zanzibar umeahidi kuongezea nguvu miradi iliyoanzishwa na wananchi.

Alisema Tasaf awamu ya tatu katika mkupuo wa pili imejipanga kukamilisha ujenzi wa kumbi mbili za mitihani za Shule ya Mahonda na Fujoni ambazo zimesita ujenzi wake kwa muda mrefu sasa.

"Nakuthibitishieni Uongozi wa Shule ya Sekondari Mahonda na Fujoni kukamilishwa ujenzi wa majengo hayo ili kuunga mkono nguvu za wananchi zinazoonekana kutaka kupotea," alisema Balozi Iddi.

Aliwaeleza wananchi, viongozi na walimu hao katika mikutano miwili tofauti kwamba mradi wa Tasaf umeendelea kufanya kazi kubwa ya kuwajengea uwezo wananchi wake hasa wale wanaoishi katika mazingira magumu.

Alieleza kwamba yapo mafanikio mengi kupitia mradi huo na kupelekea Zanzibar kupaa kimataifa iliyopelekea mataifa mbali mbali duniani kuleta watendaji wao kuja kujifunza kutokana na hatua iliyofikiwa na Zanzibar.

Aliwashauri wananchi na viongozi hao pamoja na wale wa majimbo mengine kuendelea kubuni miradi ya ujenzi na kuianzisha kwa hatua ya msingi na viongozi pamoja na Serikali itakuwa tayari kuunga mkono miradi hiyo kwa maendeleo ya jamii.

Akitoa maelezo kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya Tasaf, Mkurugenzi Uratibu Shughuli za Serikali SMT na SMZ, Khalid Bakar Amrani, alisema kupitia mradi huo Zanzibar imeshapunguza ukali wa umaskini kwa asilimia 12.

# Naibu Spika: Aibu kusimuliwa historia ya Z'bar na wageni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, amesema ni aibu kusimuliwa historia ya Zanzibar na wageni kutoka nje.

Akizungumza wakati akizindua kampeni ya 'Amka na Utalii wa Ndani',iliyoandaliwa na taasisi ya 'Mwanamke Chakarika' kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii Zanzibar, alisema wakati umefika kwa jamii ya Wazanzibari na Watanzania kwa jumla, kufuta dhana kwamba utalii ni kwa ajili ya wageni kutoka nje pekee.

Aliipongeza serikali na Rais wa Zanzibar na Rais Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuanzisha dhana ya 'utalii kwa wote', pamoja na Kamisheni kwa hatua inazochukua kuitekeleza kwa vitendo.

Alisema dhana hiyo inatoa fursa kwa kila mwananchi kujitambua kwamba ni sehemu muhimu katika kuendeleza utalii nchini, ambao unaingiza asilimia 27 ya pato la nchi, sambamba na asilimia 80 ya fedha zote za kigeni zinazoingia kutokana na vyanzo mbalimbali.

Alikiri kuwa, kwa kipindi kirefu shughuli za utalii Zanzibar zimekuwa zikinasibishwa na wageni kutoka nje pekee, hali iliyofanya sekta hiyo kuonekana haijatoa fursa kwa wananchi.

Aidha, alishauri utekelezaji wa dhana ya utalii wa ndani uende sambamba na hamu ya wananchi kujifunza na kuijua historia ya maeneo mbalimbali ili wasaidie kuwaongoza wageni wanaofika nchini kwa shughuli za kitalii pale wanapohitaji taarifa zinazoihusu Zanzibar.

"Yumkini wananchi wengi bado hawazijui rasilimali na vitu vinavyowazunguka, sasa iko haja tufanye kazi kubwa kuhakikisha kila mmoja anafahamu tunu na rasilimali zilizopo nchini," alisisitiza.

Pia aliishauri Kamisheni ya Utalii kukaa pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ili kutengeneza mpango mkakati maalumu, ikiwamo kujumuisha somo la utalii kuanzia ngazi ya msingi ili watoto wakue wakielewa thamani yake, historia yao na namna utalii unavyokuza pato na uchumi.

Mbali na kutembelea maeneo na vivutio vya utalii, Naibu Spika pia alisema utalii una fursa nyingi ambazo wananchi wanaweza kuzitumia kwa kustawisha maisha yao, ikiwamo biashara za bidhaa zinazopendwa na watalii, sanaa, usafiri, huduma za afya, mapambo na nyenginezo.

Mapema, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, aliwataka vijana kuchangamkia fursa zinazopatikana katika sekta ya utalii, lakini kwa kufanya mambo yasiyokinzana na sheria za nchi au kukiuka mila na silka za Wazanzibari.

Alisema, siku zote katika jambo lenye manufaa kwa taifa, wananchi wa nchi hiyo ndio wanaopaswa kuwa mstari wa mbele katika kuiendeleza, lakini si vyema watu wenye nia mbaya kupotosha dhana ya utalii kwa wote kwa maneno au kwa vitendo.

# Ashauri wigo zaidi tamasha la vyakula

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MENEJA wa Jumuiya ya Muungano wa Maradhi yasiyoambukiza Zanzibar, Haji Hamad Fundi, ameishauri kamati inayoandaa Tamasha la vyakula vya Asili linalofanyika Kijiji cha Makunduchi kila mwaka, kupanua wigo na kulifanya la wilaya na hatimae Zanzibar nzima.

Alisema vyakula vya asili, vilivyokuwa vikitumiwa na wazee wa zamani, ni kinga kubwa ya kujiepusha na maradhi yasiyoambukiza kwani havina kemikali ambazo ni miongoni mwa vichocheo vya maradhi hayo.

Meneja Haji alieleza hayo katika Shule ya Makunduchi alipokuwa akitoa ripoti ya utafiti wa maradhi yasiyoambukiza uliofanywa wakati wa tamasha la vyakula vya asili lililofanyika Agosti mwaka jana katika kijiji hicho.

Alisema dhana iliyojengeka kuwa maradhi yasiyoambukiza yanawapata zaidi watu wenye kipato cha juu hivi sasa haipo kutokana na wananchi kubadili utaratibu wa maisha na kupenda zaidi kutumia vyakula vya mafuta.

Aliwaeleza wananchi wa Makunduchi kuwa kwa mujibu wa utafiti uliofanywa kupitia mradi maalumu wa kuwajengea uwezo wanajamii katika kujikinga na kudhibiti maradhi yasiyoambukiza, imebainika wapo wananchi wanayo maradhi ya kisukari na shinikizo la damu katika kijiji hicho.

Aliwataka wananchi kujenga utamaduni wa kupima afya zao kila baada ya kipindi kujua afya zao ili waweze kupatiwa ushauri mapema na kufanya mazoezi kwa vile ni moja ya tiba ya maradhi hayo.

Aidha, aliwashauri wananchi wanaopatikana na maradhi yasiyoambukiza kutumia dawa wanazopewa na madaktari kwa ukamilifu kwani hakuna njia mbadala ya kutibu maradhi hayo.

Wakieleza kufaidika na mradi huo, Mzee Ali Hassan na Maryam Haji Manzi walisema wananchi wamepata uelewa mkubwa juu ya maradhi yasiyoambukiza ikiwamo kujua sababu zake, njia za kujikinga na athari zinazoweza kumpata mgonjwa wa maradhi hayo.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Night of terror
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Documentary
22:00 Kipindi Maalum: Tatu mzuka
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Kipindi Maalum: TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY**
05:30 Uwanja wa Ma0zoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Illegal sisters
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Illegal sisters 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)

## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## Mchekeshaji ashinda urais Ukraine

**KIEV,** Ukraine

MCHEKESHAJI Volodymyr Zelensky, ameshinda ushindi wa kishindo katika uchaguzi wa rais nchini Ukraine uliofanyika juzi na kupongezwa na viongozi wengi duniani.

Matokeo hayo yanaangaliwa kama maamuzi ya raia waliochoshwa na ufisadi uliotawala katika taifa hilo pamoja na hali duni ya maisha.

Zelensky ambaye uzoefu wake pekee wa kisiasi ni kuigiza kama rais katika kipindi cha televisheni, ameshinda rais aliyekuwa madarakani, Petro Poroshenko kwa kunyakua asilimia 73 ya kura zote zilizopigwa.

Poroshenko amepata asilimia 24 ya kura, na kupoteza madaraka kwa Zelensky mwenye umri wa miaka 41, huku asilimia 42 ya masanduku ya kura yakiwa yameshahesabiwa.

Ni matokeo ya kustaajabisha ikizingatiwa jinsi kampeni yake ilivyoanza kama mchezo.

Ujumbe wake uliwavutia wananchi wa Ukraine ambao walikuwa wamechoshwa na udhalimu katika jamii, ufisadi na vita vya mashariki mwa nchi hiyo kati ya serikali na waasi wanaotaka kujitenga ambao wanaungwa mkono na Urusi.

Nyota huyo wa mchezo wa kuigiza wa televisheni kwa jina la mtumishi wa watu, sasa atakamata hatamu ya madaraka na kuliongoza taifa lenye idadi ya watu wapatao milioni 45.



"Kamwe sitowaangusha. Ninaweza sasa kuziambia zile nchi zote zilizowahi kuwa za kisovieti tuangalieni sisi! chochote kile kinawezekana!'," Zelensky aliwaambia wafuasi wake waliokuwa na furaha akiwa katika makao makuu ya kampeni yake.

Matamshi hayo huenda mlengwa ikawa ni nchi jirani ya Urusi, ambako Rais wake Vladimir Putin aliyeko madarakani kwa zaidi ya miaka 20 na wengine wengi wamekuwa wakiufuatilia uchaguzi huo kwa ukaribu.

Pongezi za ushindi wa Zelensky, zilimiminika kutoka barani Ulaya na kwengineko. Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, na wa Poland, Andrzej Duda walimpongeza kwa njia ya simu rais huyo mteule.

Katibu Mkuu wa jumuiya ya kujihami (NATO), Jens Stolenberg na Rais wa Baraza la Ulaya, Donald Tusk wamesema wanategemea kuendeleza ushirikiano kati yao.

"Tunampongeza Rais-mteule Volodymyr Zelensky," uliandika Ubalozi wa Marekani Ukraine katika ukurasa wake wa Twitter.

Kampeni zake hazikuwa na mihadhara ya kijadi, badala yake mchekeshaji huyo alikuwa na hafla za vichekesho, pamoja na kuwavutia wapiga kura kupitia mitandao ya kijamii. **DW**

# Waandamanaji wasitisha mazungumzo na jeshi

**KHARTOUM,** Sudan

WAANDAMANAJI Sudan wamesema kuwa hawatambui utawala wa kijeshi uliyochukua uongozi wa nchi hiyo baada ya kumpindua kiongozi wa muda mrefu wa nchi hiyo, Omar al-Bashir.

Wanadai kuwa baraza la kijeshi lililobuniwa baada ya Bashir kutimuliwa ni mwendelezo wa utawala wake.

Maelfu ya waandamanaji wamepiga kambi nje ya makao makuu ya kijeshi mjini Khartoum wakisubiri kutangazwa kwa baraza jipya la kiraia litakalochukua madaraka.

Wakati huohuo serikali ya kijeshi ya Sudan limewaamuru waandamanaji hao kuondoa vizuwizi walivyoweka barabarani katika mji mkuu wa Khartoum mara moja ili kuruhusu usafirishaji wa bidhaa muhimu.

**Kwa sasa majenerali wa baraza la kijeshi tayari wameanza kazi na wamepata uungwaji mkono kutoka Saudi Arabia na milki za Kiarabu.**

Jeshi liliwahi kutoa agizo kama hilo lakini waandamanaji walikataa kutii amri hiyo.

Hata hivyo, msemaji wa waandamanaji hao, Mohamed al-Amin alisema kuwa baraza la kijeshi ni mwendelezo wa utawala wa zamani na kuapa kuendelea na maandamano.

Umati mkubwa wa watu bado unaendelea kuandamana katika barabara za mji kuu wa Sudan, Khartoum. Waandamaji hao wako mbioni kubuni vuguvugu la upinzani linalopigania utawala wa kiraia.

Viongozi wa mandamano hayo walitarajiwa kutangaza wanachama wao wa baraza la kiraia litakaloongoza Sudan hadi taifa hilo litakapoandaa uchaguzi wa kidemokrasia.

Hatua hiyo imezua gumzo kwamba huenda makundi kadhaa yanayoongoza maandamano hayo yametofautiana kuhusu suala la sera na nyadhifa zitakazobuniwa.

Kwa sasa majenerali wa baraza la kijeshi tayari wameanza kazi na wamepata uungwaji mkono kutoka Saudi Arabia na milki za Kiarabu.

Kampeni ya kumuondoa madarakani Bashir iliongozwa na chama cha wataalamu nchini (SPA) ambacho kimetoa pendekezo la kubuniwa kwa baraza la kiraia kuongoza nchi hiyo kwa kipindi cha mpito. **BBC**



Raia wa Sri Lanka akilia baada ya ndugu zake kufariki kutokana na mlipuko uliotokea kanisani na kuua watu zaidi ya 290. **PICHA: REUTERS**

# Waliofariki Sri Lanka wafikia 290

**COLOMBO,** Sri Lanka

RAIS wa Sri Lanka, Maithripala Sirisena, ametangaza hali ya dharura kuanzia saa sita usiku Jumatatu kufuatia shambulizi la kigaidi kwenye makanisa na hoteli za kifahari lililotokea siku ya Pasaka.

Hadi kufikia jana idadi ya waliofariki kutoka na milipuko hiyo ilifikia 290.

Taarifa ya Kitengo cha habari cha serikali ya Sri Lanka ilisema: "Serikali imeamua kutangaza sheria inayolenga kuzuia ugaidi ambayo itaanza kuheshimiwa kuanzia siku ya jumatatu"

Taarifa hiyo lifafanua kuwa hatua hiyo itahusiana tu na shughuli za kuzuia ugaidi, na haitaingilia uhuru wa watu wa kutoa mawazo yao.

Msemaji wa serikali mjini Colombo, Rajitha Senaratne, alisema kuwa serikali ya Sri Lanka inaamini kuwa kundi lenye itikadi kali la nchini humo lijulikanalo kama NTJ ndilo limefanya shambulizi hilo na kusema kuwa uchunguzi ulikuwa ukifanyika kuangalia iwapo kundi hilo lilipata usaidizi kutoka nje ya nchi.

Nyaraka zilizoonwa na shirika la habari la AFP zinaonyesha kuwa polisi wa Sri Lanka ilitoa onyo Aprili 11, mwaka huu kwamba shirika la kijasusi la nchi ya kigeni lilikuwa limeripoti kwamba NTJ ilikuwa ikiandaa njama ya kushambulia makanisha na ubalozi wa India.

Kundi la NTJ, siku za nyuma liliwahi kuhusishwa na kufanya uharibifu kwenye sanamu za madhehebu ya Buddha.

Chanzo cha habari kutoka jeshi la polisi kimeeleza kuwa watu 24 wameshakamatwa wakishukiwa kuhusika na mashambulizi ya milipuko hiyo.

Kufuatia shambulizi hilo, Sri Lanka ilifunga mitandao mingi ya kijamii, ikiwamo Whatsapp na Facebook, hatua inayodhihirisha kupungua kwa imani katika kampuni hizo mbili kubwa za kimarekani, kuweza kuchuja taarifa za uchochezi.

Mitandao hiyo miwili pamoja na Instagram imeshutumiwa kusambaza habari za uongo. Mtandao wa twitter haukuathiriwa na hatua hiyo.

Serikali ilihofu kuwa kuenea kwa ujumbe wenye hasira kungechochea ghasia zaidi nchini Sri Lanka, kisiwa ambacho wakazi wengi wa Wabudha, lakini pia yakiwapo makundi makubwa ya Waislamu, Wakristo na Wahindu. Historia ya kisiwa hicho kimekuwa kikikumbwa na vurugu za kidini.

Hii si mara ya kwanza kwa Sri Lanka kuifunga mitandao ya kijamii. Machi 2018 serikali ya nchi hiyo iliizuia kwa wiki nzima mitandao ya Whatsapp, Facebook na mitandao mingine, kwa hofu kwamba ilikuwa ikiendeleza kampeni ya chuki dhidi ya waislamu katika jimbo la katikati mwa nchi hiyo. **DW**

# Wafungwa kujenga nyumba za polisi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amesema katika ujenzi wa nyumba za makazi ya askari polisi watakuwa wanatumia wafungwa, wanafunzi wa Veta pamoja na fundi wa mitaani ili kuepusha gharama kubwa za ujenzi.

Alibainisha hayo alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa nyumba 10 za askari polisi Shinyanga Mjini, ambazo zimejengwa kwa kutumia wafungwa, wanafunzi wa Veta na mafundi wa mitaani, na kutumia gharama ndogo kiasi cha Sh. milioni 225.

Alisema amefurahishwa sana na mbinu ambayo wameitumia Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga kwa ujenzi wa nyumba hizo, ambazo zimetumia gharama ndogo tofauti na wangetafuta makandarasi ambapo zingeweza kutumia hata shilingi bilioni moja.

"Kwenye ujenzi wa nyumba hizi 10 za askali polisi nimejifunza kitu... kumbe tunaweza kutumia fedha ndogo sana kumaliza tatizo la makazi ya askari wetu hapa nchini, nitamwagiza IGP Simon Sirro ujenzi wote za nyumba za polisi watumie wafungwa, wanafunzi wa Veta pamoja na mafundi wa mtaani," alisema Lugola.

Naye Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya ujenzi, Cosmas Peter Taligura, alisema walipewa na Rais John Magufuli Sh. milioni 225 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tisa za askali polisi mjini humo, lakini kutokana na ubanaji wa fedha hizo ikabidi waongeze nyumba nyingine na kufikisha 10.



Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Itilima wilayani Kishapu, Mkoa wa Shinyanga, Athumani Katundu, akitoa mada kwa wanawake na watoto kuhusu namna ya kutunza ushahidi dhidi ya matukio ya ukatili wa kijinsia, ili kupunguza matukio hayo ama kuyamaliza kabisa, **PICHA: MARCO MADUHU**

# Viongozi CCM waagizwa ubora wa miradi

**Na Dege Masoli,** KOROGWE

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, Nassoro Malingumu, amewaagiza viongozi wa chama hicho kuanzia ngazi ya kata kuhakikisha ubora wa viwango vya miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao unafikiwa na thamani halisi ya fedha za wavuja jasho zinazotolewa.

Malingumu alitoa agizo hilo jana alipotembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya hiyo unaotekelezwa katika Kijiji cha Makuyuni kilichopo nje mwa Mji wa Korogwe.

Aliwataka viongozi wa chama hicho kutojitenga na shughuli za kimaendeleo na kijamii na kwamba wajibu wa kufuatilia na kusimamia miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao unatokana na CCM kubeba dhamana pamoja na mambo mengine ni kuhakikisha kodi ya wananchi inatumika ipasavyo.

Kwa upande wa wataalamu, alisema ni watu muhimu kwa taifa na kutokana na umuhimu huo, aliwataka watumie vikaokazi kama sehemu ya kujitathmini na kupata majibu ya matokeo ya malengo waliyojiwekea na kufanya hivyo kutawapa majibu ya matokeo ya kazi zao za kila siku kwa jamii pamoja na kutambua mapungufu na kuyafanyiakazi ili kuongeza tija zaidi.

# Hekima haikutumika shauri la CAG Assad

INATOKA UK. 4

Kwa hiyo, bado tutaendelea kuwa na wabunge kwa sababu hata wabunge kutoka Zanzibar wanaendelea kuwapo ndani ya chama.

**SWALI:** Wapo wabunge wa CUF ambao wameweka wazi kwamba watamfuata Maalim Seif alikokwenda. Wewe ni kiongozi mkubwa ndani ya CUF. Ni hatua zipi ambazo mmepanga kuchukua kwa wabunge wa aina hiyo?

**SAKAYA:** Taasisi yoyote makini, haiwezi kukubaliana na kitendo cha mtu kuvaa kofia yake huku anashabikia kwingineko. Taasisi ya aina hiyo haitakuwapo kwa sababu wabunge wote ndani ya Bunge hili kuna mbunge mmoja tu wa ACT (Zitto Kabwe).

Mbunge yeyote aliyeingia bungeni kwa tiketi ya CUF halafu akaendelea kushabikia kwamba yeye anamuunga mkono Maalim Seif, atashughulikiwa.

**SWALI:** Kuna dhana kwamba viongozi wa CUF sasa mnatumiwa na serikali ya CCM. Kuna ukweli upi kuhusu tuhuma hizi?

**SAKAYA:** Sijui ni kwa namna gani tunatumiwa na serikali. Mimi nimekuwa mbunge wa upinzani kwa miaka 13 sasa, na ukifuatilia michango yangu tangu nimekuwa mbunge hadi leo, nabaki kutetea haki za wanyonge na penye udhaifu nakosoa, penye mazuri napongeza. Ndivyo nilivyo tangu nimeingia bungeni.

Hata leo (juzi) nilikuwa na swali humo bungeni, nadhani umelisikia vizuri. Sasa, kama ni mbunge unayetumiwa na serikali, sidhani kama unaweza kuuliza swali kama lile. Nimesema wazi pasi na shaka kwamba majibu yaliyotolewa na serikali hayaonyeshi umakini wa kufanyia kazi suala la matumizi ya mifuko ya plastiki nchini.

Nimetoa sababu na nikaeleza. Sasa sijui natumikaje. Labda wangetueleza tunatumikaje maana sisi hatujui. Unatumika ili mambo ya serikali yapite au unatumikaje?

Jambo la tofauti kidogo ambalo mimi nimelifanya ni kuunga mkono bajeti kuu ya serikali. Bajeti ya mwaka juzi na bajeti ya mwaka jana niliunga mkono kwa kutoa sababu.

Pale ninapoona kuna mambo nilikuwa natamani yafanyike, yamefanyika na ninayaona yanaendelea kufanyika, hata kama hayajakamilika, maadam kuna dhamira ya kuyafanya, napongeza na kutia nguvu ili yafanyike vizuri zaidi.

Utawala wa awamu ya nne niliuponda mwanzo - mwisho kwa sababu tulikuwa hatuendi kabisa. Tulikuwa hatusogei kabisa. Huku bungeni kila mmoja alikuwa analia, waziri analia, naibu waziri analia, mkurugenzi analia, mbunge unalia, ni vilio kwa kwenda mbele.

Lakini, katika utawala huu, madam Rais John Magufuli anafanyia kazi yale ambayo tulikuwa tunayatamani kwa maana ya kufanyia kazi changamoto ya kukithiri kwa rushwa, kutowajibika kwa watendaji wa serikali, rasilimali zetu kuchotwa huku tukiendelea kuwa ombaomba, kukosekana kwa nidhamu ya utumishi na kulipa mishahara kwa watumishi hewa, kwanini usimpongeze?

Tulikuwa tumezoea kuona mahabusu wanaingia dagaa, papa wanabaki huku mitaani wanatamba, lakini sasa tunashuhudia watu wakubwa wanaingia mahabusu.

Wapo watu wakubwa wameingia mahabusu hadi leo wako huko, walikuwa hawagusiki. Kuna mfanyabiashara mkubwa alikuwa hajawahi kukanyaga hata mlango wa mahabusu tangu azaliwe, lakini awamu hii kakanyaga, tena na kulala humo kwa siku kadhaa.

Sasa, kama unaona mambo haya, kama unaona kuna miradi mikubwa inatekelezwa, kwanini usipongeze kama Mtanzania mzalendo? Vita dhidi ya rushwa na dawa za kulevya tunaipigana waziwazi.

Kuna watu walikuwa wanafanya biashara ya dawa za kulevya tunawafahamu, leo wanaogopa hata kusafiri kwenda kuchukua. Kosa letu nafikiri ni kupongeza kazi inayofanyika, tunaonekana tunatumika.

Nakuhakikishia huku si kutumika, mimi ni Mtanzania mzalendo, ninapoona jambo zuri linafanyika ndani ya nchi yangu, nitalitambua lakini pia nakosoa sana bila kuogopa napoona kuna udhaifu mahali popote.

**SWALI:** Huoni kwamba dhana hii ya kuonekana unatumiwa na serikali, inaiweka hatima yako ya kisiasa mahali pabaya?

**SAKAYA:** Binafsi naona inanijengea heshima. Watanzania wa leo si wa zamani, wana uwezo mkubwa wa kupambanua mambo. Haya nayoyaona mimi, siyaoni peke yangu. Hata wa kule chini wanayaona.

Mtanzania wa pale Kaliua ukimwambia serikali hii iliyoko madarakani haifanyi chochote, hakubali kwa sababu anaona hata ndani ya Jimbo la Kaliua kuna mambo yanayofanyika.

Kaliua tulikuwa hatuna maji kabisa. Hatukuwa na mradi wa maji wa aina yoyote, leo kuna miradi huko. Kaliua leo inanufaika na fedha ya makusanyo ya halmashauri ambayo ilikuwa inatafunwa.

Leo Kaliua kwa kutumia fedha zake za ndani, za walipakodi wake, kuna hospitali ya kisasa inajengwa, tunajenga jengo kubwa la mama na mtoto, kuna miradi ya barabara inaendelea.

Hayo si mimi tu ninayeyaona, hata wao wanayaona. Kwa hiyo, hata wakisikia hapa bungeni unaongeza kazi zinazofanyika, hawakushangai badala yake wanaongeza kukuamini, ndiyo maana nakwambia inawezekana naongezwa sifa kwenye nafasi yangu ya kuendelea kuwa mbunge.

**SWALI:** Ukipata dakika moja leo kuzungumza na Maalim Seif, utamshauri jambo gani la muhimu?

**SAKAYA:** Ningemwambia 'Mzee ni vema ukatunza heshima yako'. Maalim Seif amekuwa kiongozi mkubwa kwenye nyadhifa mbalimbali, amewahikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, amekuwa Katibu Mkuu wa chama chetu kwa miaka 15. Kuna hadhi fulani unafikia, kuna umri unafikia, mambo yako inabidi uyafanye tofauti na mtu ambaye hajafikia hadhi uliyonayo.

Kwa hiyo, nikikutana naye, nitamwambia 'japokuwa umeondoka CUF kwenda ACT, ni vizuri ukalinda heshima na hadhi yako. Uendelee kutambua kuwa ulikuwa ndani CUF na CUF imekujenga mpaka hapo ulipofikia hadi ukawa Makamu wa Kwanza wa Rais'.

Haya yanayoendelea ya kutaka kuiua CUF si sawa. Adui wetu ni CCM, ni chama tawala, ambacho tunataka tuking'oe madarakani ili wananchi wapate huduma bora zaidi. Tunapoanza kushambuliana sisi kwa sisi si sawa kabisa.

# HABARI MICHEZO




## VIRGIL VAN DIJK

**KUZALIWA:** JULAI 8, 1991
**LIPOZALIWA:** BREDA, UHOLANZI
**KIMO:** MITA 1.93
**UZITO:** KILO 92
**URAIA:** UHOLANZI
**KLABU:** LIVERPOOL F.C
**NAFASI:** BEKI WA KATI
**JEZI:** NAMBA 4

# MARCELO: SINA MPANGO WA KUMFUATA RONALDO




**MADRID,** Hispania

MARCELO amesisitiza kwamba hana mpango wa kuondoka Real Madrid kipindi cha majira ya joto, licha ya ripoti kumhusisha na mpango wa kutaka kuungana na Cristiano Ronaldo kule Juventus.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil amejikuta kwenye wakati mgumu kupenya katika kikosi cha kwanza hapo kwenye dimba la Bernabeu, huku Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 22, akiwa amechukua nafasi hiyo.

Hata hivyo, baada ya kurudi kwa Zinedine Zidane kama kocha, Marcelo amejikuta tena kwenye kikosi hicho, na kupuuzia uvumi wa kuhamia Italia.

Alisema akiiambia beIN SPORTS: "Kila mmoja anajua kwamba nina furaha hapa, na huwa naionyesha kila wakati nikiwa kwenye mazoezi na timu nikiwa nimevalia jezi ya timu hii.

"Kuna mambo mengi yanayosemwa kutoka nje. Sifikirii kuhusu hilo. Madrid ni nyumbani kwangu na wote wanaonijua mimi wanajua ukweli wake."

Akiwa amejiunga na klabu hiyo akitokea Fluminense mwaka 2007, Marcelo alikuwa akitajwa kama mrithi wa gwiji wa zamani wa Real, Roberto Carlos, na tangu hapo amecheza jumla ya mechi 482 kwa klabu hiyo, akifunga mabao 36.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ameshinda mataji manne katika nyakati tofauti na ameshinda mara nne taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

# Sarri: Kufika fainali Uefa ni rahisi kuliko Carabao



**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, amedai kwamba, kufika fainali ya Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya ni rahisi kuliko kufika hatua kama hiyo kwenye Kombe la Carabao.

Blues hao wamejikuta wakiwa kwenye vita ya kuwania kufuzu kwenye mashindano hayo makubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Ulaya msimu ujao, huku pia wakikabiliwa na mchezo dhidi ya Eintracht Frankfurt kwenye nusu fainali ya Kombe la Europa mwezi ujao.

Akizungumza kabla ya mchezo wake wa jana Jumatatu dhidi ya Burnley wa Ligi Kuu, Sarri alionekana kutoona umuhimu wa michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akilinganisha na ile ya Carabao.

Raia huyo wa Italia akinukuliwa na Gazeti la Daily Mirror, alisema: "Ligi Kuu England ni ngumu mno.

"Kufika fainali ya Kombe ya Ligi, tulilazimika kucheza dhidi ya Liverpool, Tottenham na halafu Manchester City kwenye fainali. "Ni rahisi kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Lakini kwenye Ligi ya Europa huwezi kutarajia lolote kwa sasa na si kitu rahisi. Tutajaribu kwa njia zote."

# *Barcelona yaamua kuachana na Rashford*

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imeondoa uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford kipindi cha majira ya joto wakihofia kuwa atawagharimu fedha nyingi.

Huku 'Blaugrana' hao wakiwa na mpango wa kutafuta mrithi wa mshambuliaji wake, Luis Suarez, Rashford alikuwa mmoja wa nyota waliokuwa kwenye rada zao, na bado hajakubali kuongeza mkataba mpya pale Old Trafford.

Hata hivyo, Barcelona sasa wanapanga kuangalia kwingineko huku Gazeti la Express likidai kwamba hakuna uwezekano wa Rashford, ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 150.

Pamoja na ada yake kuwa kubwa, Barcelona ilikuwa tayari kumpa ofa Rashford ya mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki, ambao ungemfanya kuwa mmoja kati ya wachezaji wanne wanaolipwa zaidi pale Camp Nou, akiwa sawa na Philippe Coutinho na nyuma ya Suarez, Ousmane Dembele na Lionel Messi.

Uhamisho wa Rashford ungekuwa wa gharama na hivyo Barcelona sasa inaona uwezekano wa kutafuta mchezaji sehemu nyingine, licha ya kuvutiwa na kiwango chake kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.


Hata hivyo, bado wataendelea kumtupia jicho mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye bado anavutana na United kusaini mkataba mpya.

Mkataba wake wa sasa unamalizika kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2020, ingawa 'Mashetani Wekundu' hao wana kipengele cha kumuongezea mkataba wa mwaka mmoja zaidi, kama walivyofanya kwa David de Gea.



## HABARI MICHEZO

# 'POGBA MWENYEWE HAWEZI UTD'




**MANCHESTER,** England

TIMU ya Manchester United, haitasimama kwa faida ya Paul Pogba, amesisitiza kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Tangu kurudi kwake pale Old Trafford kwa pauni milioni 89.3 kutoka Juventus mwaka 2016, mjadala kuhusu mchango wa kipaji cha Pogba umekuwa ukiibuka na kupotea.

Uhusiano wake na kocha wa zamani, Jose Mourinho ulisababisha kocha huyo kutimuliwa na kiungo huyo wa Ufaransa kurudi kwenye ubora wake wakati Solskjaer alipopewa mikoba ya kuinoa timu hiyo.

Hata hivyo, kama ilivyo kwa wachezaji wenzake kiwango cha Pogba kimekuwa kwenye mjadala baada ya United kupoteza mechi tano na kushinda mbili kati ya saba zilizopita kwenye mashindano yote.

Ripoti ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, kuhusishwa na mpango wa kutakiwa na Real Madrid imeleta sitofahamu na Solskjaer amebainisha kwamba ataendelea kumtaka Pogba kufanya vitu tofauti uwanjani kama ambavyo anaombwa na timu.

"Kila mmoja amekuwa na mtazamo wake kuhusu Paul. Na bila shaka pamoja na Paul, tumekaa chini na kujadiliana kuhusu nafasi yake uwanjani," amesema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tunajua kwamba anaweza kucheza kama namba 10 au sita, tunajua kwamba anaweza kucheza nafasi nyingine nyingi, kama alivyotufanyia mwanzo na kama alivyofanya akiwa na Juventus.

# Henderson: Tutapigania ubingwa Liver hadi mwisho

**LIVERPOOL,** England

JORDAN Henderson amesema Liverpool itaendelea kupigania ubingwa wa Ligi Kuu England, EPL hadi dakika za mwisho za msimu kuelekea wiki ngumu kwa wote, 'Wekundu' hao na Manchester City.

Liverpool Jumapili ilishinda 2-0 ugenini dhidi ya Cardiff City na kurejea kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, lakini kikosi cha Pep Guardiola kina mechi moja mkononi dhidi ya mahasimu zao Manchester United itakayochezwa kesho, Jumatano.


Ushindi wa bao 1-0 City iliyoupata dhidi ya Tottenham katika Uwanja wa Etihad mwishoni mwa wiki ulikuwa wa 10 mfululizo kushinda kwenye EPL na mabingwa hao watetezi wanajua kombe bado lipo mikononi mwao kama hawatadondosha pointi yoyote katika mechi zao nne za mwisho.

Lakini Henderson alisisitiza kuwa wataendelea kuamini katika nafasi zilizopo wakati wakitafuta kutwaa ubingwa wa EPL kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi kupita.

"Ni matokeo makubwa kwetu na tunataka kuendelea kupigana hadi mwisho kuendelea kushinda mechi," nahodha huyo wa Liverpool aliiambia tovuti ya klabu yao baada ya ushindi dhidi ya Cardiff.

"Ni ladha tofauti kwetu na nilidhani tulipenya vizuri. Tunapaswa kuendelea kuamini, kuendeleza kujiamini kwetu na kushinda mechi nyingi kadri tuwezavyo.

"Tulijua itakuwa ni mechi ngumu, ilikuwa joto kali, hivyo tunajua itakuwa ni vigumu, lakini kwa kuwa mkweli, ilikuwa sawa kwa timu zote."







# Mbappe amaliza uvumi kutua Real

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, ameelezea kwamba atabakia katika klabu yake msimu ujao huku akimaliza uvumi kwamba atahamia Real Madrid kipindi cha majira ya joto.

Kocha Zinedine Zidane ameripotiwa kwamba ni shabiki mkubwa wa mchezaji huyo na amekuwa akihusishwa na mpango wa kumsajili Mbappe ili kukiimarisha kikosi chake.

Hata hivyo, akizungumza na Canal+ baada ya PSG kupata ushindi wa 3-1 dhidi ya Monaco Jumapili, Mbappe alimaliza uvumi kuhusu majaliwa yake ya baadaye klabuni hapo.

Alisema: "Nabakia PSG. Nilijiunga na mradi wa PSG. Nina furaha kwamba Zizou amerudi Real Madrid. Nitaaangalia mechi kama shabiki."

Kuhusishwa kwa 'Los Blancos' kumchukua nyota huyo kulikolezwa zaidi baada ya Mbappe kumbwatukia kocha Thomas Tuchel wiki iliyopota.

Akizungumza na Canal+ baada ya kichapo cha kushitukizwa cha 5-1 kutoka kwa Lille, Mbappe alihoji uwezo wa kikosi chake na kutupa shutuma kwa kocha huyo.

Mbappe aliachwa kwenye mchezo uliofuata dhidi ya Nantes, kabla ya kurudi kwenye kikosi dhidi ya timu yake ya zamani Jumapili kwenye mchezo wa Ligue 1 na kufunga hat-trick.

# DO… O ZA SOKA MA… ETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: MAN UNITED HAITAMBEBA SANCHEZ

●●● Kama klabu hututawabeba wachezaji, sizungumzi kuhusu Alexis pekee, kila mmoja yupo...

**Manchester,** England

OLE Gunnar Solskjaer amemuonya Alexis Sanchez na wachezaji wenzake wa Manchester United kwamba 'Mashetani Wekundu' hao hawatabeba wachezajji wakati huu akitazama kuisuka upya klabu hiyo ili kurejesha heshima yao ya kutwaa makombe.

**Kocha huyo wa United hakutaka kuficha lolote kutokana na kuamini kwamba kuisaidia United kutoa changamoto ya kuwa kinara wa Ligi Kuu na michuano ya Ulaya itakuwa ni mradi wa muda mrefu hapo Old Trafford.**

Kipigo mara tano katika mechi saba zilizopita za ugenini kimepeperusha kung'ara kwa Solskjaer alikokuwa akifurahia mafanikio yake ya mechi zake za mwanzo hapo Old Trafford.

Mustakabali wa baadaye wa Sanchez upo mashakani kuelekea mwishoni mwa msimu wakati United ikijengwa upya na hasa kutokana na mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Chile kuendelea kuhaha kuwa fiti tangu alipojiunga na klabu hiyo akitokea Arsenal Januari mwaka jana.

Na wakati akiwa na mabao mawili tu kwa jina lake kwa msimu huu mzima, Sanchez anaweza kujikuta akiwa ahitajiki, ingawa ukubwa wa mshahara wake - ambao unaripotiwa kuwa zaidi ya pauni 400,000 kwa wiki kunaweza kuthibitisha kuwa kizuizi.

Na Solskjaer ameonya kuwa kila mchezaji katika kikosi hicho anapaswa kuonyesha kuwa na kiu ya mafanikio.

"Kama klabu hatuwezi kubeba wachezaji," Solskjaer alisema. "Kila mmoja anahitaji kuchukua umiliki, kuendelea kujizatiti, kuonyesha njaa ambayo unahitaji kuwa bora binafsi na kama timu.

"Sizungumzi kuhusu Alexis pekee. Kila mmoja yupo katika uhitaji kama huo. Lakini kama tunazungumza kuhusu Alexis, hakuwa na bahati na majeraha.

"Tangu mimi nilipoingia, amekuwa majeruhi wa muda mrefu ambayo hayakuwa yenye manufaa kwake. Baadhi ya wachezaji wengine wamekuwa majeruhi pia. Lakini nimeona tabia tuliyo nayo. Ninatazama ni nani ninapaswa kumbakisha, nani anapaswa kuondoka. "Alexis amekuwa na kipaji kizuri wakati anapokuwa katika ubora wake. Sasa tunamtaka kuonyesha ubora wetu."

United Jumapili ilitembezewa kipigo cha mabao 4-0 katika Uwanja wa Goodison Park kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Everton wakati huu ikipigania kumaliza nafasi nne za juu.

## ZISIKUPITE

### MSHAHARA KUMZUIA POGBA

MSHAHARA anaohitaji kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, 26, unaweza kuthibitisha kuwa kizuizi kwa kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa kutua Real Madrid. ***(AS)***

### COUTINHO KUMRITHI HAZARD

CHELSEA inamtaka kiungo wa Barcelona, Mbrazil Philippe Coutinho, 26, kama mbadala wa mshambuliaji Mbelgiji Eden Hazard, 28, ambaye anatarajiwa kujiunga na Real Madrid. ***(Calciomercato)***

### HENRY KUINOA N. Y RED BULLS

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Arsenal, Thierry Henry, 41, ambaye pia aliwahi kuinoa Monaco, yupo katika mazungumzo ya kuwa kocha mpya wa New York Red Bulls ya Ligi Kuu Marekani, MLS. ***(Sky Sports)***

### MBAPPE AIKANA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe, 20, amekanusha tetesi kuwa anaweza kujiunga na Real Madrid baada ya kufunga hat-trick dhidi ya klabu yake ya zamani ya Monaco. ***(Goal.com)***

### PHELAN KUMPISHA CARRICK

MANCHESTER United ipo tayari kumpa ofa Mike Phelan, kuwa mkurugenzi wa ufundi - na kumpandisha cheo kiungo Michael Carrick kuwa kocha msaidizi. ***(Mail)***

### LIVER, ARSENAL KWA HAZARD

LIVERPOOL na Arsenal zipo tayari kutoa ofa kwa kiungo wa Borussia Monchengladbach, Mbelgiji Thorgan Hazard, 26. ***(Star)***

### CAVANI HANA UHAKIKA PSG

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Uruguay, Edinson Cavani, 32, hawezi kuthibitisha kwamba mustakabali wake wa baadaye upo na PSG. ***(Canal+, via Goal)***

### YANOGEWA NA BAKAYOKO

AC Milan inaonekana inataka kuufanya mkataba wa mkopo wa kiungo Mfaransa Tiemoue Bakayoko, 24, kuwa wa kudumu, lakini itahitajika kuilipa Chelsea takribani pauni milioni 30 ili kumpata. ***(Calciomeracto)***

### PEPE AMULIKWA LIVERPOOL

LIVERPOOL imewasiliana na Lille kuhusu kumsajili mshambuliaji Muivory Coast Nicolas Pepe, 23. ***(Le10 Sport, via Mirror)***

### BENITEZ HAKIJAELEWEKA

MUSTAKABALI wa baadaye wa kocha wa Newcastle, Rafa Benitez, upo mashakani licha ya ahadi ya kupewa pauni milioni 100 za kutumia sokoni majira ya joto. ***(Star)***

### GIROUD KURUDISHWA UFARANSA

RAIS wa Nice, Gauthier Ganaye, amesema miamba hiyo inaweza kufunga safari ya kwenda kumsajili mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud. ***(Goal.com)***

### KUACHANA NA NEWCASTLE

MSHAMBULIAJI wa Newcastle, Mhispania Ayoze Perez, 25, amefunguka kuhusu kuondoka majira haya ya joto. ***(Mirror)***

# Kocha Coastal ashangaa matokeo Ligi Kuu Bara

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union ya jijini Tanga, Juma Mgunda, amesema Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ni ngumu na inawaweka "roho juu" makocha, wachezaji na mashabiki wa timu zote hapa nchini.

Mgunda aliliambia gazeti hili kwa njia ya simu kuwa anauona ugumu wa ligi utakwenda hadi mechi ya mwisho kutokana na baadhi ya mechi kuwa na matokeo yanayoumiza kwa upande mmoja na mwingine kushangaza.

"Angalia Simba kaja hapa Mkwakwani katufunga, kaenda Bukoba naye kafungwa, lakini sisi (Coastal Union) tulipokwenda Kaitaba tulipata ushindi na tukafurahia pointi tatu tulizoondoka nazo," alisema Mgunda.

Alisema kikubwa ni wachezaji kuendelea kujituma ili kufikia mahali pazuri, ingawa kikanuni ni lazima kuwe na bingwa wa ligi na timu zitakazoshuka daraja kutokana na kufanya vibaya.

Mapema mwezi ujao, Coastal Union itasafiri kwenda Dar es Salaam kuifuata Simba katika mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Mei 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa.

Ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayofanyika kila mwaka inatarajiwa kumalizika ifikapo Mei 28, mwaka huu kwa mechi 10 kuchezwa katika viwanja mbalimbali hapa nchini.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yangas | 32 | 23 | 5 | 4 | 51 | 23 | 74 |
| 2. Azam | 32 | 19 | 9 | 4 | 49 | 19 | 66 |
| 3. Simba | 24 | 19 | 3 | 2 | 51 | 10 | 60 |
| 4. Mtibwa Sugar | 32 | 14 | 6 | 12 | 33 | 24 | 48 |
| 5. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 6. Ndanda | 32 | 11 | 10 | 11 | 22 | 30 | 43 |
| 7. Kinondoni MC | 31 | 9 | 15 | 7 | 32 | 22 | 42 |
| 8. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 9. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 10. Singida United | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 11. Kagera Sugar | 32 | 9 | 12 | 11 | 28 | 33 | 39 |
| 12. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 19 | 26 | 39 |
| 13. Stand Utd | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 14. Mbeya City | 31 | 10 | 7 | 14 | 30 | 34 | 37 |
| 15. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 16. Alliance | 32 | 9 | 10 | 13 | 23 | 33 | 37 |
| 17. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara Utd | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# MKUDE AWATOA HOFU MASHABIKI WA SIMBA

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

BAADA ya timu yake kupoteza mchezo uliopita dhidi ya Kagera Sugar, kiungo wa Simba, Jonas Mkude, amesema wamejipanga kuongeza umakini na bila kuwadharau wenyeji wao, Alliance FC.

**Simba inatarajia kushuka ugenini kuwavaa Alliance FC katika mchezo wake wa 25 wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza leo.**

Mabingwa hao watetezi wako jijini hapa tangu juzi na nyota wake wote wamekuwa wakifanya mazoezi mepesi na magumu, katika muda tofauti.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkude, alisema hakuna mechi rahisi katika Ligi Kuu, lakini timu itakayokuwa na nidhamu uwanjani ndiyo yenye asilimia kubwa ya kupata pointi tatu muhimu.

Mkude alisema hakuna timu inayoingia uwanjani kwa ajili ya kufungwa, ila anayeruhusu kufanya makosa ndiyo yanaweza kuwagharimu na hatimaye kupoteza mchezo.

"Tumekuja kupambana, mechi zetu hizi zimekuwa zinatizamwa sana na wapinzani wetu, tukifanya vizuri itatusaidia kutetea ubingwa tunaoushikilia na hiyo ndiyo mipango yetu," alisema nyota huyo ambaye alianzia timu ya vijana ya umri chini ya miaka 20 maarufu Simba B.

Baada ya mechi ya leo, Simba itaendelea kubaki jijini hapa kwa ajili ya kuwavaa KMC FC ya Dar es Salaam katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba pia.

Simba ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo inayoshirikisha jumla ya timu 20 na Yanga yenye pointi 74 ndio vinara wakati African Lyon, zote za jijini Dar es Salaam inaburuza mkia.




Mesut Ozil (kulia), akiifungia Arsenal bao la kwanza wakati wakikubali kipigo cha mabao 3-2 dhidi ya Crystal Palace, kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi. **PICHA: DAILY MAIL**

# *Ubingwa Ligi Kuu Z'bar hautabiriki*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya Ligi Kuu Zanzibar kubakisha michezo miwili kwa kila timu kabla ya msimu kumalizika, hadi sasa hakuna timu ambayo inaweza kutabiriwa kuibuka bingwa na kuiwakilisha Zanzibar kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Katika ligi hiyo hadi sasa kuna ushindani mkubwa ambapo timu mbili za juu zinafungana alama sawa huku zikitofautiana tu kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Kinara wa ligi hiyo kwa sasa ni Mabaharia wa KMKM ambao wana alama 74 huku nafasi ya pili ikishikiliwa na Maafande wa Kvz wote wenye apointi 74 wakizidiwa tu kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Hata hivyo, nafasi ya tatu inakishikiliwa na Maafande wa Zimamoto ambao wana alama 73.

Awali akizungumza na gazeti hili kocha msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema matarajio yake makubwa ni kuhakikisha ananyakuwa ubingwa wa Zanzibar msimu huu.

Alisema michezo iliyobaki atakiandaa kikosi chake ili ahakikishe hapotezi mechi yoyote huku wakilenga kupachika mabao mengi ili wasije ruhusu kuukosa ubingwa huo kutokana na tofauti tu ya mabao.

Kwa upande wake Kocha wa KVZ, Sheha Khamis, alisema anatamani kunyakuwa ubingwa, lakini katika dakika hizi za mwisho chochote kinaweza kutokea hususan katika matokeo.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea lea Jumanne kwa kupigwa michezo mitatu katika viwanja viwili, kwenye Uwanja wa Amaan saa nane timu ya Chuoni itakipiga na Mlandege, huku saa kumi uwanjani hapo JKU na Malindi zikitoana jasho wakati katika Dimba la Mau, Zimamoto na Jang'ombe Boys nao watakuwa wakiwania alama tatu muhimu.

Michezo
Jumanne Aprili 23, 2019
Nipashe



Solskjaer: Man United haitambeba Sanchez UKURASA 30

PENALTI...



Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, akiangushwa chini na beki wa Cardiff City, Sean Morrison, na kuzawadiwa penalti katika kipindi cha pili kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Cardiff City juzi. Liverpool ilishinda 2-0. **HABARI UK. 29**

# Aussems aichambua Alliance, aitaja Yanga

## Asema haitakuwa mechi rahisi Simba itakapoivaa Kirumba leo huku akieleza lengo lake...

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

HAWATOKI! Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema anahitaji matokeo chanya tu na si kitu kingine katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Alliance FC unaotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, jijini hapa, huku akieleza lengo lao ni kutaka kuikamata Yanga na Azam kileleni.

**Simba ambao ni mabingwa watetezi wa ligi hiyo, watashuka ugenini hapa Mwanza wakiwa na jeraha la kuchapwa mabao 2-1 na Kagera Sugar katika mchezo uliopita ambao ulichezwa mjini Bukoba Jumamosi iliyopita.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems alisema pia anatarajia kukutana na ushindani katika mchezo huo kutokana na wachezaji wa Alliance FC sasa kuimarika tofauti na walivyokutana nao kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza.

Aussems alisema pamoja na changamoto hiyo anaamini wachezaji wake hawatawadharau kutokana na nafasi waliyopo na kujiandaa kucheza kwa bidii zaidi ili wapate ushindi na kuikaribia Yanga na Azam FC ambao wako juu katika msimamo wa ligi.

Mbelgiji huyo alisema hakuna mechi nyepesi katika ligi hiyo kwa upande wake na timu nyingine kutokana na kila mmoja kuhitaji kutimiza malengo yake.

"Tunatarajia kukutana na ushindani, tulishinda mechi ya kwanza kule Dar es Salaam, ilikuwa ni ya mapema, sasa kila timu wachezaji wake wameimarika na wanajiandaa kuonyesha soka la kiwango kizuri, lakini hii haitufanyi tuache kuwaza pointi tatu, ila tunawaheshimu sana Alliance," alisema Aussems.

Naye Kocha Mkuu wa Alliance FC, Malale Hamsini, alisema wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo ambao wamejipanga kukutana na ushindani kutoka kwa mabingwa hao watetezi.

"Simba ni timu yenye jina kubwa, tunawaheshimu kwa hilo, lakini sisi pia tumejiandaa kutafuta pointi tatu, ingawa najua haitakuwa rahisi kwangu na kwao pia, sina majeruhi na kila mchezaji wa timu yangu anaamini anaweza kujituma na kuisaidia klabu kupata ushindi," alisema Malale.

Aliongeza kuwa endapo wachezaji wake wataheshimu nafasi zao, hapo hana wasiwasi wa kupata ushindi katika mchezo huo.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Simba yenye pointi 60 ilipata ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya wenyeji wao wa mchezo wa kesho wenye pointi 37, lakini wakiwa wamecheza mechi 32.

# Mchakato uchaguzi Yanga waanikwa

**Na Mwandishi wetu**

MCHAKATO wa uchaguzi Mkuu wa Klabu ya Yanga ya jijini Dar es Salaam unaelekea vema huku sasa kamati ikiwa inasubiri kupokea pingamizi mbalimbali kwa wagombea kama zitawasilishwa.

Yanga ambayo viongozi wake waliokuwa madarakani walijiuzulu wote, inatarajia kufanya uchaguzi mkuu ifikapo Mei 5, mwaka huu hapa jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Ally Mchungahela, aliliambia gazeti hili kuwa maandalizi ya uchaguzi huo yanakwenda vema na hiyo imetokana na pande zote za klabu hiyo kuridhia mchakato huo.

Mchungahela (pichani chini) amewataka wanachama wa klabu hiyo kutoka sehemu mbalimbali nchini kujiandaa kuchagua viongozi wao ambao watawaongoza kwa muda mwingine wa miaka minne.

"Hadi sasa mchakato wa uchaguzi unakwenda vema na kalenda tuliyoitoa ndio inayofuatwa, hakuna jipya wala mabadiliko," alisema mwenyekiti huyo.

**WACHEZAJI MAWINDONI**

Katika hatua nyingine Kikosi cha Yanga kitarejea kuanza mazoezi leo kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC utakaochezwa Aprili 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema kuwa wanatarajia kufanya mazoezi asubuhi na uamuzi wa kuingia kambini ili kujiwinda na mchezo huo bado haujatolewa.

Saleh alisema kuwa benchi la ufundi la timu hiyo litakuwa na kikao ili kufanya uamuzi wa wapi kikosi chao kitaweka kambi kwa sababu wanajua mechi hiyo ni moja ya michezo itakayoamua nafasi yao ya kuwania ubingwa.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002